DCB COMMERCIAL BANK

# MKUTANO MKUU WA 20 WA WANAHISA NA TAARIFA YA BENKI KWA MWAKA 2021.

*Mkombozi wa kweli*

TUNASHEREHEKEA Miaka 20 YA MAFANIKIO

# YALIYOMO


Taarifa ya Kampuni .......... 01
Orodha ya vifupisho vya maneno.......... 03
Kuhusu Benki yetu.......... 05
Taarifa ya Mkutano Mkuu wa 20 wa Wanahisa.......... 15
Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa 19 wa Wanahisa.......... 17
Barua ya Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi.......... 25
Barua ya Mkurugenzi Mtendaji .......... 29
Wasifu wa Wakurugenzi.......... 33
Safu ya Uongozi.......... 36
Taarifa ya fedha kwa mwaka ulioisha 2021 .......... 55
Taarifa za gawio la mwaka ulioisha Tarehe 31 Disemba 2021.......... 68
Kuthibitisha na Kuidhinisha uteuzi wajumbe wa Bodi .......... 69
Kupokea na kuridhia pendekezo la malipo ya ada kwa wajumbe wa Bodi .......... 71
Kuteua mkaguzi huru wa hesabu kwa mwaka wa fedha 2021 .......... 73
Kupanga tarehe ya Mkutano Mkuu wa ishirini na moja.......... 74
Kusherekea Miaka Ishirini.......... 75
Kufunga mkutano .......... 79
Viambatanisho.......... 80
(A) Orodha ya Kesi .......... 85
(B) Orodha ya Mahudhurio ya Mkutano Mkuu wa kumi na Tisa.......... 85




# TAARIFA ZA KAMPUNI

## OFISI ILIYOSAJILIWA

Jengo la DCB House Kitalu Na. 182 - R
Magomeni Mwembechai,
S.L.P 19798 Dar es Salaam.

## BENKI

Benki Kuu ya Tanzania
S.L.P 2939
Dar es Salaam

Benki ya Biashara ya NMB
S.L.P 9213
Dar es Salaam

Benki ya Biashara ya D.T.B
S.L.P 115
Dar es Salaam

Benki ya Biashara ya CRDB
S.L.P 268
Dar es Salaam

## KATIBU WA KAMPUNI

Ms Regina Mduma
Jengo la DCB House
Kitalu Na. 182 - R
Magomeni Mwembechai
S.L.P 19798
Dar es Salaam

## WAKAGUZI

PricewaterhouseCoopers
369 Mtaa wa Toure,
Oysterbay,
S.L.P 45
Dar es Salaam

# VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| **AGM** | Mkutano Mkuu wa Mwaka |
| **ALCO** | Kamati ya Mali na Dhima |
| **BOT** | Benki Kuu ya Tanzania |
| **DSE** | Soko la Hisa la Dar-es-Salaam |
| **EAD** | Kadirio la hasara ya mikopo isiyolipika ya benki |
| **ECL** | Matarajio ya baadaye ya hasara ya mikopo |
| **EPS** | Mapato kwa hisa |
| **FTE** | Wafanyakazi wa muda mrefu |
| **FVOCI** | Thamani sawa kupitia mapato mengine |
| **IASB** | Bodi ya Viwango ya Uhasibu ya Kimataifa |
| **IESBA** | Bodi ya Viwango ya Maadili ya Kimataifa ya Wahasibu |
| **IFRS** | Viwango vya Kimataifa vya Taarifa za Fedha |
| **ISA** | Viwango vya Kimataifa vya Ukaguzi |
| **LC** | Barua za mikopo |
| **LDR** | Mkopo kwa uwiano wa Amana |
| **LGD** | Hasara itokanayo na mkopo usiolipika |
| **OCI** | Mapato mengine |
| **PD** | Uwezekano wa mkopo kutokulipika |
| **POCI** | Mali zinazotarajiwa kuingiza hasara |
| **SICR** | Ongezeko Kubwa la Hatari ya Mikopo |
| **SGL** | Ukopaji wa Vikundi |
| **SME** | Wafanyabiashara wadogo na kati |
| **SMR** | Kiwango cha Chini cha Amana cha Kisheria |
| **SPPI** | Malipo ya Kianzio na Riba |
| **SPV** | Kampuni ya makusudio maalum |
| **TMRC** | Taasisi ya Mikopo ya Nyumba ya Tanzania |
| **TZS** | Shilingi ya Kitanzania |
| **USD** | Dola ya Marekani |
| **ROUA** | Haki ya Matumizi ya Mali |





# KUHUSU BENKI YETU

## Dhumuni letu

Kutoa huduma bora za kifedha ambazo ni rafiki, zenye ubora na ubunifu kwa wateja wetu na wakati huohuo tukichangia maendeleo kiuchumi na kijamii huku tukiwaongezea wanahisa thamani kwenye uwekezaji wao.

## Dira yetu

Dira ya Benki ya Biashara ya DCB ni kutoa huduma pendwa za kifedha nchini Tanzania.

## Dhima yetu

Kutoa huduma za kifedha kwa Wateja wetu ambazo ni rafiki kutumia, zenye ubora na ubunifu wa hali ya juu , huku tukichangia katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii na kuwaongezea wanahisa thamani kwenye uwekezaji wao.

## Maadili yetu

**Uadilifu -** Tunajivunia kuwa na ujasiri wa kutenda na kusema yale yanayofaa.

**Ushirikiano Kazini -** Tumejitolea kwa dhati kufikia malengo ya pamoja yaliyojikita katika mawasiliano ambayo ni ya wazi na ya ukweli wakati tukizingatia kuthaminiana na kusaidiana.

**Heshima -** Tunathamini na kuhamasisha maoni tofauti kutoka kwa wafanyakazi na wadau wetu.

**Utii na Uwajibikaji -** Tunawajibika na matokeo yote, yawe ya kushindwa au kufanikiwa na kuepuka kulaumiana.

**Ubunifu na Uvumbuzi -** Sisi ni waanzilishi wa mifumo ya ubunifu na mfano wa kuigwa wa namna bora za kuendesha shughuli zetu.

**Umahiri -** Tuna azma ya dhati ya kuhakikisha kuwa tunajenga mazingira bora.

## Kanuni za utoaji huduma zetu

**Maarifa –** Uelewa thabiti wa huduma za Benki ya DCB.

**Urafiki -** Usikivu makini na uungwana.

**Kujali Muda -** Tunatoa huduma kwa haraka na kutimiza ahadi zetu.

**Kuongeza Thamani -** Kujituma kwa ziada na kutoa suluhisho za changamoto.

## Tabia zetu

**Kasi ya Utendaji -** Tuko makini na tunayapa kipaumbele majukumu yetu.

**Matumizi Sahihi ya Muda –** Tunaheshimu na kuthamini muda.

**Umiliki –** Tunatambua kuwa sote tunawiwa kuwajibika.

# NGUVU YETU

## Bodi ya Wakurugenzi
Uongozi wa Benki thabiti wenye uwezo na nguvu na sifa stahili.

## Benki ya Biashara
Benki ya kwanza kupanda hadhi kutoka benki ya jamii hadi benki ya kibiashara.

## Mtaji
Benki ya Biashara ya DCB inamtaji thabiti wa kiasi cha shilingi bilioni 24 na fedha za wanahisa zinazofikia kiasi cha shilingi bilioni 30.2 ambazo zinatuwezesha kupanua wigo wa uwekezaji na ukuaji wa benki.

## Mizania
Benki ina zaidi ya shilingi bilioni 190 na jumla ya Mali zaidi ya shilingi bilioni 190.

## DSE
Benki ya kwanza Tanzania kusajiliwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam.

## Wanahisa wa Uhakika
UTT - AMIS • Jiji la Dar es salaam • Manispaa ya Ilala • NHIF • Manispaa ya Kinondoni • Manispaa ya Temeke • Manispaa ya Ubungo • Manispaa ya Kigamboni • Wananchi

## Ushirikiano Thabiti
UTT - AMIS • Jiji la Dar es salaam • Manispaa ya Ilala • NHIF • Manispaa ya Kinondoni • Manispaa ya Temeke • Manispaa ya Ubungo • Manispaa ya Kigamboni •

## Mtandao
Huduma za benki zinapatikana nchi nzima
- Matawi 9
- Vituo zaidi ya 1,500 vya utoaji wa mikopo kwa wafanya biashara wadogowadogo
- Huduma za Kidigitali
- ATM zaidi ya 270 za Umoja Switch
- ATM zinazotumia Visa card duniani

## Huduma za Kidijitali
Mtandao thabiti wa kidijitali unaotumiwa na zaidi ya asilimia 70 ya wateja wetu nchi nzima.
•DCB Pesa •DCB Malipo •Huduma ya QR Code
•GePG - mfumo wa kielektroniki wa kufanya malipo ya serikalini

## Nafasi Yetu Sokoni
- Wigo mpana wa Wateja zaidi ya 200,000
- Miaka 20 ya kuhudumia wajasiriamali wadogo na wa kati zaidi ya 400,000.
- Mikopo yenye thamani ya zaidi ya shilingi Bilioni 120 kwa wafanyakazi na wafanyabiashara.

## Chapa Imara
Chapa imara ya uzoefu wa zaidi ya miaka 20 ya kutoa huduma bora kwa wateja yenye zaidi ya wafanyakazi 250 wenye weledi, ujuzi na uzoefu.

## Mikakati Thabiti
Mikakati thabiti ya kufikisha huduma kwa watanzania wote hususani wafanya biashara wa kipato cha chini na cha kati wanaojumuisha sehemu kubwa ya uchumi Tanzania.



# MATAWI NA VITUO VYETU VYA HUDUMA



## MATAWI NA VITUO VYETU VYA HUDUMA




## Ufunguo

- Matawi
- Vituo Vya Huduma
- Vituo vya huduma vijavyo



# BIDHAA NA HUDUMA ZETU



## Lamba Kwanza

Ni akaunti maalumu nayomuwezesha mteja kuwekeza hadi miaka miwili na kupata riba ya hadi asimilia 10% ya amana atakayo wekeza. Riba inalipwa kila mwanzo wa mwezi. *#ChangamkiaFursaWekezaNaDCB*



## DCB Digital

Hii ni akaunti ya akiba inayofunguliwa kupitia simu ya mkononi na kukuwezesha kufanya miamala yote. Ukiwa na akaunti hii huna haja ya kufika tawini. Jinsi ya kujiunga *Piga *150*85#.*



## Internet Banking

Fanya huduma zote za kibenki kwa urahisi na usalama ukiwa na DCB Internet Banking popote pale ulimwenguni. *#MwendoKidijitali*



## International Money Transfer

Tuma na pokea fedha kutoka mahali popote duniani. Hamisha pesa kwa haraka na salama kwa SWIFT na TISS,ukiwa ndani na nje kwa dola za marekani(USD), Euro(UER),Randi ya Afrika kusini(ZAR),Shilingi ya kenya(KES) na shilingi ya Uganda(UGX).*#DuniaKijiji*



## Akaunti ya Mshahara

Ni akaunti ya akiba inayomwezesha mteja kupitisha malipo ya mshahara kutoka kwa mwajiri (Taasisi au Kampuni) kuja benki ya DCB. Mwajiri anatakiwa awe amesaini makubaliano maalumu na benki ya DCB.




## Akaunti ya Wahi

Ni akaunti ya akiba inayomuwezesha mteja kujiwekea kiwango cha Akiba kila mwezi kwa mpango wa miezi 3, 6, 9,12 au 24 kulingana na mahitaji yake.
*#HatuaKwaHatua*



## Akaunti ya Wastaafu

Ni akaunti ya akiba ambayo inafunguliwa na muajiriwa mwenye umri wa miaka 50 na kuendelea au mstaafu. Akaunti hii inamuwezesha kuweka akiba kwa ajili ya kujiandaa na kustaafu. Akaunti hii haina makato yoyote.
*#StaafuKifahali*



## Akaunti ya Skonga

Ni akaunti maalum inayompa fursa mteja ya kuweka akiba kila mwezi ili kutimiza malengo yake, huku akiwahakikishia watoto elimu hadi chuo kikuu. Akaunti hii inakupa fursa ya kuchagua kiwango na muda wa kuweka.
*#ElimuMpangoMzima*





## GEPG

GePG ("Government e-Payment Gateway") ni Mfumo wa kielektroniki unaowezesha ukusanyaji wa fedha za umma kielektroniki Serikalini. Lipa kodi za TRA, TPA, TCAA, MUHIMBILI, NIC na MANISPAA YA KINONDONI kupitia DCB DCB PESA, DCB JIRANI, Internet Banking na matawi ya DCB nchi nzima.
*#UhuruWaMalipo*



## Akaunti ya Royal Saving

Furahia uhuru wa kubenki ukiwa na akaunti ya Royal. Akaunti hii inakuwezesha kupata kadi ya VISA Black Infinite.



## Mikopo ya Vikundi

Mikopo hii hutolewa kwa mtu mmoja mmoja anayejiunga katika kikundi cha watu watano wenye biashara endelevu.



## Mkopo wa Executive Loan

Pata mkopo wa hadi kiasi cha Shillingi Milioni 50 (Tsh 50,000,000) ndani ya masaa 48.



# TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI WA WANAHISA



## Agenda

**1.** Kufungua mkutano

**2.** Kuridhia agenda ya Mkutano Mkuu wa Ishirini.

**3.** Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 19 wa wanahisa uliofanyika tarehe 12 Juni 2021

**4.** Kupokea na kuridhia

4.1.Taarifa za wakurugenzi za mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2021
4.2. Taarifa ya mkaguzi huru na ya hesabu zilizokaguliwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2021

**5.**Taarifa ya gawio kwa mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2021

**6.** Kupokea na kuridhia pendekezo la malipo ya ada kwa wajumbe wa Bodi

**7.** Kupokea taarifa ya Kujiuzulu na wajumbe wapya wa Bodi

**8.** Kuteua mkaguzi huru wa hesabu kwa mwaka wa fedha 2022.

**9.** Kupanga tarehe ya Mkutano Mkuu wa ishirini na moja

**10.** Mengineyo

**11.** Kufunga mkutano

## Maelezo

**1.** Mwanahisa atakayehudhuria Mkutano Mkuu anatakiwa kujigharamia mwenyewe na aje na hati ya hisa iliyotolewa na Soko la Hisa la Dar-es-Salaam pamoja na kitambulisho chake cha kupiga kura au cha taifa au hati ya kusafiria.

**2.** Mwanahisa anayestahili kuhudhuria na kupiga kura lakini akashindwa kuhudhuria kikao, anaweza kuwasilisha Jina la Mbadala wake (Proxy) kwa Katibu wa benki kabla ya saa 08:00 mchana Ijumaa ya tarehe 10 Juni 2022 katika ofisi za Makao Makuu zilizoko jengo la DCB, Magomeni Mwembechai au kwa barua pepe kupitia shareholders@dcb.co.tz au info@dcb.co.tz. Kwa makampuni, fomu inapaswa kuwa katika lakiri ya kampuni mwanahisa.

3. Kufungwa kwa orodha (Register) ya wanahisa - tarehe 7 Juni 2022

4. Mapendekezo ya wanahisa yawasilishwe kwenye ofisi za makao makuu zilizoko jengo la DCB Magomeni Mwembechai au kwa barua pepe kabla ya saa 8.00 mchana siku ya Alhamisi tarehe 9 Juni 2022.

5. Vitabu vyenye taarifa ya hesabu ya mwaka 2021 pamoja na fomu ya mwakilishi mbadala (proxy) vitapatikana ofisi za makao makuu zilizoko jengo la DCB, Magomeni Mwembe chai na katika matawi yote na ofisi za madalali wa Soko la Hisa la Dar-es-Salaam na kwenye tovuti ya benki www.dcb.co.tz kuanzia tarehe 3 Juni 2022.

KWA IDHINI YA BODI,

***Regina Mduma***
Katibu wa Kampuni
Mei 2022.



# MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TISA

## MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TISA WA WANAHISA WA DCB COMMERCIAL BANK PLC ULIOFANYIKA TAREHE 12 JUNI 2021 KWA NJIA YA MTANDAO NA KATIKA UKUMBI WA DIAMOND JUBILEE, DAR ES SALAAM.

### Waliohudhuria

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Maharage Chande | Mwenyekiti wa Mkutano |
| 2. | Bi. Zawadia Nanyaro | Mjumbe wa Bodi |
| 3. | Bw. Godfrey Ndalahwa | Mkurugenzi Mtendaji |
| 4. | Bi. Regina M. Mduma | Katibu wa Kampuni |

### a. Wanahisa Wakuu

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Matao Alexander Adolfu | Halmashauri ya Jiji la Dar-es-Salaam |
| 2. | Bw. Matao Alexander Adolfu | Halmashauri ya Manispaa ya Ilala |
| 3. | Bw. Onesmo Rafael Monga | Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni |
| 4. | Bw. Justine Evance Massangya | Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo |
| 5. | Bw. Salum Ally Papon | Halmashauri ya Manispaa ya Temeke |
| 6. | Bw. Charles Lawisso | Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni |

### b. Wanahisa kutoka Taasisi

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bi. Pamela Nchimbi | UTT – Amis |
| 2. | Bw. Alexander Sanga | National Health Insurance Fund (NHIF) |

### c. Wanahisa binafsi Orodha imeambatanishwa

### d. Waalikwa

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Richi Mandi | Benki Kuu ya Tanzania (BOT) |
| 2. | Bi. Bw. Alex G. Mgongolwa | Mwanasheria Mshauri wa DCB |
| 3. | Bi. Mariam Mtunguja | Mamlaka ya Masoko ya Mtaji na Dhamana (CMSA) |
| 4. | Bw. Leonard Kameta & Davis Kyando | Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) |
| 5. | Bw. Costa Andrew | Mkaguzi Huru – Pricewaters Coopers |
| 6. | Bw. Cletus Kayuga | Mkaguzi Huru - Pricewater Coopers |
| 7. | Bw. Cliff Maregeli | Mjumbe wa Bodi anayependekezwa |
| 8. | Dr. Amina Baamary | Mjumbe wa Bodi |

### UTANGULIZI:

Mkurugenzi alishukuru watu wote waliofika katika Mkutano Mkuu na wale wote waliojiunga kwa njia ya mtandao. Pia alitambulisha Bodi ya wakurugenzi na wageni waalikwa. Mkurugenzi alikaribisha wanahisa, wageni waalikwa, wakurugenzi wa Bodi ya DCB na wafanyakazi wa benki ya DCB kwenye Mkutano Mkuu wa kumi na tisa wa benki ya biashara ya DCB.

## KUFUNGUA MKUTANO:

Katibu wa benki akishirikiana na Mwanasheria Mshauri wa benki walithibitisha kwamba akidi imetimia kutokana na maudhurio ya wanahisa wenye hisa zenye thamani ya asilimia 75 ya hisa za benki. Wanahisa walihudhuria kikao ukumbini na kwa njia ya mtandao. Baada ya hapo mnamo saa 4 kamili asubuhi, Mwenyekiti wa Bodi alifungua rasmi Mkutano Mkuu wa Kumi na tisa wa Wanahisa wa Benki ya Biashara ya DCB.

## KURIDHIA AGENDA YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TISA.

Wajumbe waliridhia agenda za Mkutano Mkuu wa Kumi na tisa kama zilivyoorodheshwa kwenye taarifa ya Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 19 wa benki.

## KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA KUMI NA NANE

Wajumbe walithibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na nane uliofanyika tarehe 27 Juni 2020.

## KUPOKEA NA KURIDHIA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA MKUTANO MKUU WA KUMI NA NANE ULIOFANYIKA TAREHE 27 JUNI 2020.

Taarifa ya utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa na Mkutano Mkuu wa kumi na nane wa Mwaka, iliwasilishwa na Wajumbe walipokea na kuridhia utekelezaji wa maagizo hayo.

## TAARIFA YA WAKURUGENZI NA TAARIFA YA HESABU ZILIZOKAGULIWA KWA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DISEMBA, 2020.

Wajumbe walipokea taarifa ya wakurugenzi iliyoeleza kwamba benki ilipata faida ghafi ya shilingi bilioni 1.02, ambayo ni asilimia 48 chini ya kiwango cha mwaka wa fedha uliotangulia (2019). Wajumbe walijulishwa kwamba kama ilivyokuwa kwa makapumpuni mengine, benki ilipata athari zinazosababishwa na janga la Uviko 19 katika nusu ya kwanza ya mwaka. Athari hizo ni pamoja na benki kupoteza fursa kadhaa za kibiashara zilizopelekea kushuka kwa kiwango cha ukusanyaji wa marejesho ya mikopo na ongezeko la tengo la mikopo chechefu kama inavyoagizwa na Benki Kuu.

Wajumbe walijulishwa kwamba benki imeshuhudia ukuaji mkubwa wa mapato kupita miaka mitatu iliyopita. Taarifa iliyotolewa ni kwamba pato halisi lililopatikana mwaka 2020 lilikuwa TZS bilioni 17.67, ambayo ni asilimia 5.5 juu zaidi ya mwaka 2019. Pato la faida ghafi lilifikia TZS bilioni 22.67 (asilimia 15.72) juu zaidi ya shilingi bilioni 19.59 za mwaka 2019, wakati pato lisilogharimiwa lilifikia kiwango cha TZS bilioni 4.48 ambayo ni asilimia 8.6 zaidi ya mwaka uliopita. Mikopo ghafi kwa wateja ilikua hadi kufikia TZS bilioni 104.8, ambayo ni ongezeko la asilimia 12 ikilinganishwa na mwaka 2019.

Wanahisa walijulishwa kwamba amana za wateja zimekua kwa asilimia 26, ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 13 kilichopatikana mwaka 2019. Gharama za amana ziliongezeka kutoka asilimia 6.4 mwaka 2019 hadi asilimia 7.7 mwaka 2020 ikiwa ni ongezeko la shilingi bilioni 1.4.

Wajumbe walijulishwa kwamba ada na malipo mengine yaliongezeka kwa asilimia 9 na kufikia shilingi bilioni 4.48, ikiwa ni asilimia 24 chini zaidi ya ongezeko lililopatikana mwaka 2019. Wajumbe walifahamishwa kuwa, benki imejikita katika kuboresha bidhaa na huduma zake ili kutoa suluhu la mahijati ya wateja wake kupitia maboresho ya huduma zinazotolewa kwa njia ya kidigitali. Taarifa ilitolewa kuwa benki ina mfumo wa kibenki wa intaneti na huduma za kadi za VISA.

Wajumbe walifahamishwa kwamba pato la fedha za kigeni limeongezeka kwa asilimia 83 kufikia shilingi milioni 152.

Taarifa ilitolewa kwamba pamoja na changamoto zilizopo, benki ilifanikiwa kushusha kiwango cha mikopo chechefu kutoka asilimia 14 mwaka 2019 hadi kufikia asilimia 11.67 mwaka 2020. Benki ilikusanya TZS bilioni 1.9 (2019: shilingi bilioni 2.1) kutoka mikopo chechefu, hii ilipelekea ongezeko la faida na kupunguza tengo la mikopo chechefu kwa kiasi cha shilingi bilioni 1.26. Ongezeko hili la faida lilipunguzwa na gharama ya TZS milioni 829 iliyotokana na kufutwa kwa madeni yasiyolipika na yaliyotimiza vigezo vya kufutwa kisheria.

Wanahisa walijulishwa kwamba mwezi Desemba 2020, Bodi ya Wakurugenzi na menejimenti ya benki ilipitisha mpango-mkakati mpya wa miaka mitano ulioainisha taswira ya mafanikio yafuatayo: kuendelea kupata faida hadi kufikia pato la thamani la 18.9% kutoka 6% mwaka 2019, kuendelea kushusha kiwango cha mikopo chechefu hadi kufikia chini ya 5%, kuendelea kupunguza kiwango cha mapato na matumizi hadi 55%, kuwa benki ya kidigitali, kutoa huduma kulingana na matakwa ya wateja wake, kuongeza idadi ya wateja hadi kufikia 400,000, kuongeza matawi, vituo vya huduma na wakala nchini, kuimarisha udhibiti na kuwa muajiri bora ambaye ni chaguo la wafanyakazi nchini.

Taarifa ilitolewa kwamba, DCB imendelea kulipa fadhila kwa kutumia kauli mbiu ya "Mkombozi wa Kweli". Kwa mwaka ulioishia Disemba 2020, benki imechangia kodi kwa kiasi cha shilingi bilioni 2.44 zikiwemo VAT, ushuru wa Forodha na kodi nyingine mbalimbali. Aidha benki imetoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 72 kwenye sekta mbalimbali za uchumi.

Wajumbe walijulishwa kwamba benki imeendelea kuwa kinara na kushika nafasi ya juu kwa miaka 3 mfululizo baada ya kupata tuzo za uwasilishaji bora wa mahesabu (Kundi la Huduma za Kibenki - ndogo na za kati).

Taarifa ya Bodi ya wakurugenzi ilithibitishwa na mkaguzi huru wa mahesabu kutoka kampuni PriceWatershouseCoopers (PWC), Bw. Cletus Kiyuga kwamba taarifa iliyotolewa ni sahihi, zinaonyesha hali halisi ya benki na kwamba kampuni hiyo imetoa hati safi ya mahesabu.

Wajumbe walipokea na kuridhia barua ya Mwenyekiti, ujumbe wa Mkurugenzi Mtendaji na taarifa za mahesabu zilizokaguliwa za mwaka 2020. Wajumbe waliipongeza Bodi na Menejimenti kwa kupata hati safi na faida. Pia wajumbe walitoa mapendekezo yafuatayo na kutaka ufafanuzi wa taarifa ifuatayo:

(i) Benki iendelee kujikita kwenye mpango mkakati wake.

(ii) Wajumbe walitaka ufafanuzi kuhusu ununuzi wa hisa za TMRC. Mkurugenzi mtendaji alifafanua kwamba kwa kuwa benki ni mwanahisa wa TMRC hivyo ununuzi wa hisa za TMRC ni moja kati ya matakwa ya kampuni ili uwiano wake wa uwekezaji usipungue. Kama mwanahisa, benki inapata faida ya kupata fedha kwa riba nafuu ambayo benki inatumia kutoa mikopo ya nyumba.

## KUPOKEA TAARIFA KUHUSU GAWIO LA MWAKA ULIOISHIA 31 DISEMBA 2020

Wanahisa walitaarifiwa kwamba katika hatua ya kuhakikisha kwamba sekta ya kibenki inaendelea kuendesha shughuli zake katika mazingira salama, thabiti na ya uhakika, Benki Kuu ya Tanzania ilitoa waraka unaozitaka benki na Taasisi zote za kifedha kuhakikisha kwamba uwiano wa gharama kwa mkopo hauzidi asilimia 55. Waraka huo ulieleza kwamba benki ambazo hazijafikia uwiano huo zitatakiwa kurekebisha uwiano ifikapo Desemba 2022. Aidha waraka huo umezitaka benki zote kudhibiti mikopo chechefu (NPL) na kupunguza uwiano kufikia asilimia 5. Benki Kuu imeamuru kwamba benki ambazo hazitatimiza matakwa ya waraka huo hazitaruhusiwa kulipa gawio kwa wanahisa wao na bonasi kwa wafanyakazi kuanzia tarehe ya waraka huo.

Bodi ya Wakurugenzi na Menejimenti ya benki ya DCB ilipokea agizo hilo kama changamoto yenye lengo la kuongeza ufanisi katika biashara na kuongeza mapato na hatimaye kuongeza thamani ya hisa zake. Benki iliwasilisha mpango mkakati ambapo benki yetu imeeleza hatua na jitihada itakazochukua ili kuhakikisha inatimiza uwiano unaotakiwa na muda ulioelekezwa. Wajumbe walifahamishwa kwamba benki inaendelea kufuatilia swala hili kupitia Jumuiya ya Mabenki Tanzania (TBA) ikiwa na nia ya kuomba kupewa upendeleo maalumu utakaowezesha benki kutoa gawio kutokana na faida inayopatikana huku ikiendelea kutimiza malengo ya kufikia uwiano unaokubalika na Benki Kuu.

Wajumbe walijulishwa kwamba kutokana na maagizo hayo ya kisheria, Bodi ya Wakurugenzi imependekekeza kutokulipa gawio kwa mwaka 2020. Pia Bodi ilipendekeza kuwa, faida iliyopatikana katika mwaka 2020 ijumuishwe kwenye fedha za wanahisa na kusaidia uendeshaji wa benki wakati benki inajitahidi kufikia malengo ya 2021.

Wanahisa walipokea taarifa kuhusu gawio kwa mwaka ulioishia 2020 na kuridhia kutokulipa gawio lolote kwa mwaka 2020. Wanahisa waliridhia kwamba faida iliyopatikana katika mwaka 2020 ijumuishwe kwenye fedha za wanahisa na kusaidia uendeshaji wa benki. Pia wajumbe walitoa mapendekezo na maagizo yafuatayo;

Wajumbe walipendekeza kwamba ili kuweza kutoa gawio, benki inatakiwa kuangalia mikakati yake ili iweze kupunguza gharama za uendeshaji.

Benki ilipokea pendekezo hilo na kufahamisha wajumbe yafuatayo:

(i) Agizo la Benki Kuu ni changamoto ya kisekta na sio la DCB peke yake.

(ii) Pia kuendelea kupunguza gharama za uendeshaji wake. Moja ya hatua ya kupunguza gharama za uendeshaji; benki imezindua mfumo mpya wa kidigitali ambao gharama zake ni za chini na utaiwezesha benki kufika nchi nzima kwa gharama ndogo.

(iii) Benki imeweka mikakati ili kuhakikisha kwamba inaongeza ufanisi ili kuweza kufikia malengo iliyojiwekea kwa muda muafaka. Wajumbe walikumbushwa kwamba benki ilipata hasara kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo (2015, 2016 and 2017) na kupitia mkakati mpya wa mwaka 2018 benki iliweza kutoka kwenye hasara kwenda kwenye faida, kuimarisha ukwasi na mwisho kufikia kwenye hatua ya ukuaji.

## KUPOKEA NA KURIDHIA PENDEKEZO LA MALIPO YA ADA KWA WAJUMBE WA Bodi

Bodi ilipendekeza malipo ya ada kwa Wakurugenzi yaendelee kuwa shilingi 6,000,000 kwa mwaka baada ya kodi kwa kila Mjumbe wa Bodi.

Wajumbe waliridhia pendekezo la kutoongeza ada ya Wajumbe wa Bodi.

## KUJIUZULU NA KUTHIBITISHA WAJUMBE WAPYA WA Bodi YA WAKURUGENZI

Wajumbe walifahamishwa kwamba Katika Mkutano Mkuu wa 18 wa Mwaka wanahisa walitoa Azimio la kwamba Bodi ya Wakurugenzi ifanye usaili na uteuzi wa wajumbe wawili wa Bodi ya Wakurugenzi.

Wajumbe walitaarifiwa kwamba Bodi ilifanikiwa kufanya usaili na kuwateua
Bw. Cliff N. Maregeli na Bw. David M. Shambwe kuwa wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi.

Pia wajumbe walijulishwa kwamba kutokana na kustaafu kwa aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya wakurugenzi Prof. Lucian Msambichaka mnamo tarehe 30 Mei 2020, nafasi moja katika Bodi ya wakurugenzi ipo wazi. Kutokana na changamoto zinazoikumba benki katika kufikia akidi ili kuweza kufanya vikao vyake, Bodi ilitangaza nafasi ya mjumbe wa Bodi na kamati ya Bodi ya Uteuzi ilifanya usaili na kumteua Dr. Amina A. Baamary kama mjumbe wa Bodi. Wajumbe waliomba kumuidhinisha Dr. Amina Baamary kama mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi.

Wajumbe walipokea taarifa na kuidhinisha wafuatao kama wajumbe wa Bodi baada ya kuthibitishwa na Bank kuu ya tanzania:-
i. Bw. Cliff N. Maregeli
ii. Bw. David M. Shambwe
iii. Dr. Amina A. Baamary

## KUTEUA MKAGUZI HURU WA HESABU KWA MWAKA WA FEDHA 2021
Wajumbe walijulishwa mchakato uliofanywa wa kumchagua mkaguzi huru wa hesabu kwa mwaka 2021. Baada ya kushindanisha makampuni tofauti ya kimataifa na yenye uwezo Bodi ilipendekeza PriceWaterhouseCoopers (PWC) kuteuliwa kama mkaguzi huru kwa mwaka 2021 kwa gharama za shilingi 128,000,000. Wajumbe waliridhia pendekezo hilo.

## KUPANGA TAREHE YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI
Wajumbe waliazimia kuwa Mkutano Mkuu wa Ishirini wa Wanahisa ufanyike siku ya Jumamosi, tarehe 11 Juni 2022.

## MENGINEYO
Kikao hiki hakikuwa na mengineyo.
Mkutano ulifungwa saa 7:00 mchana

| | |
|---|---|
| **Bw. Maharage Chande**<br>Mwenyekiti wa Bodi | 11 Juni 2022<br>**Tarehe** |
| **Bi. Regina Mduma**<br>Katibu wa Kampuni | 11 Juni 2022<br>**Tarehe** |



# TAARIFA YA BIASHARA YETU

- Barua ya Mwenyekiti wa Bodi
- Barua ya Mkurugenzi Mtendaji



**Bw. Maharage Chande**

*Mwenyekiti wa Bodi DCB*

# BARUA YA MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI

Ndani ya miaka 20 benki yetu ilifanikiwa kulipa gawio kwa wanahisa mara 15. Haya ni mafanikio makubwa kwa benki na wawekezaji. Benki yetu sasa imerudi katika kupata faida kila mwaka huku ikiendelea kuimarika zaidi, hivyo ni matumaini yangu kwamba benki itaanza kulipa gawio kila mwaka kama ilivyokuwa desturi yake.

**Ndugu Wanahisa:**

Kwa niaba ya Bodi ya wakurugenzi, ninayo furaha kuwakaribisha nyote katika Mkutano wa 20 wa Wanahisa wa benki yetu. Kabla sijaanza kusoma taarifa yangu nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa tena afya njema na kuweza kukutana nanyi tena. Mkutano huu utajadili maendeleo ya Benki yetu pamoja na kuadhimisha miaka 20 tangu kuanzishwa kwake, tukiangalia tulipotoka, tulipo sasa na tunakoelekea.

Ndugu wanahisa, niwahakikishie kwamba benki inaendelea vizuri na ipo imara na inaendelea kupata faida na kufanya vyema kwenye soko la hisa la Dar es Salaam.

Kama mnavyofahamu, benki ya DCB ilifungua milango yake kwa wateja kwa mara ya kwanza mwaka 2002 ilipopata leseni ya kufanya biashara kama benki ya kijamii (Community Bank). Benki yetu ilianzishwa kufuatia kilio cha wakazi wa mkoa wa Dar es Salaam baada ya kukosa huduma za kifedha hasa mikopo kwa wajasiriamali Wadogo Wadogo hasa wanawake.

Benki ilianzishwa kwa mtaji anzia wa shilingi bilioni 1.7 kutoka kwa wanahisa waanzilishi watano ambao walikuwa ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Manisapaa za Temeke, Kinondoni na Ilala pamoja na wananchi walioji-tokeza kununua hisa. Zoezi hili zima lilisimamiwa kidete na aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mh. Yusuph Makamba kulingana na maelekezo aliyopewa na Raisi wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hayati Benjamin W. Mkapa.

## Mafanikio ya miaka 20

Ndugu wanahisa, mafanikio tunayojivunia ni makubwa na ninapenda kuchukua fursa hii kuainisha baadhi ya mafanikio hayo:

Ikumbukwe kuwa DCB ilikuwa benki ya kwanza kuorodheshwa katika soko la hisa la Dar es Salaam (DSE) baada ya kutimiza vigezo na masharti ya mamlaka mbalimbali za udhibiti hapa nchini. Kuorodheshwa katika soko la hisa haikuwa tu fursa kwa umma kumiliki benki na kutengeneza faida iliyotokana na gawio pamoja na kuuza na kununua hisa, bali imekuwa fursa kubwa zaidi kwa benki kuongeza mtaji pindi unapohitajika.

Niwashukuru sana wanahisa wenzangu kwa kuendelea kushiriki katika mazoezi ya uuzwaji wa hisa jambo ambalo limesaidia kukuza mtaji wa benki yetu kutoka shilingi bilioni 1.7 hadi kufikia shilingi bilioni 30 hivi sasa. Mtaji huu umeiwezesha benki kukidhi masharti ya benki kuu ya kujiendesha kama benki ya biashara na kuiongezea benki yetu uwezo mkubwa wa kushindana katika soko.




- Mwaka 2012 benki yetu ilifanikiwa kuhuisha leseni kutoka kwenye benki ya jamii na kuwa benki kamili ya biashara ambayo imepanua wigo kwa benki yetu kuweza kushindana katika soko ikihudumia wateja wadogo, wa kati na wakubwa. Katika kufanikisha hayo, benki iliweza kufungua matawi 9, vituo 5 vya huduma na mawakala zaidi ya 700 maeneo tofauti nchini. Benki yetu pia haikuwa nyuma katika kuanzisha mifumo ya kidijitali ambayo kwa sasa ndio ushindani wa soko ulipo, hivyo mnamo mwaka 2016, benki ilianza kutoa huduma za kibenki kwa njia ya simu na mtandao na imeendelea kuboresha huduma hizo kadri teknolojia inavyozidi kubadilika.

Huduma hizi za Kidijitali zimewezesha kufikia wateja wengi zaidi kwa muda mfupi hivyo kurahisisha shughuli za utoaji huduma.

Ndugu wanahisa, wakati benki inaanzishwa ilijikita kwenye kuhudumia wafanyabiashara wadogo na wateja binafsi wa jiji la Dar es salaam ambapo kiwango cha utoaji mikopo kwa mteja mmoja kilianzia shilingi 200,000 hadi shilingi milioni 5. Kwa kipindi cha miaka 20, benki yetu inajivunia kutoa jumla ya mikopo yenye thamani isiyo pungua trilioni 1 ambayo imenufaisha watanzania wasiopungua 400,000. Aidha baada ya kuboresha leseni yake kiwango cha utoaji mikopo kiliongezeka hadi kufika uwezo wa kukopesha bilioni tano kwa mteja mmoja. Kadhalika, mikopo hiyo sasa hunufaisha wafanyabiashara wote yaani wadogo, kati na wakubwa bila kusahau wateja binafsi popote nchini.

Leo ninayo furaha kutamka kwenu kwamba, wateja hao waliokuwa wakikopa shilingi 200,000 wameweza kupanua mitaji yao na hivyo kuwawezesha kumudu majukumu yao ikiwemo ada za watoto, ujenzi wa nyumba na mengineyo. Baadhi yao wameweza kuongeza uwezo wa kukopesheka kutoka shilingi 200,000 hadi kufikia shilingi milioni 100 na zaidi.

Ndugu wanahisa, haya ni mafanikio makubwa kwa benki na kwa wateja wetu kwani tunaamini lengo la waasisi la kuhakikisha watanzania wanapata huduma wanayostahili na kwa wakati limefanikiwa. Benki inaendelea kuboresha huduma ikihakikisha wananchi wengi zaidi wananufaika.

Wakati tunaanza wateja walikuwa takribani 6,530 ambao wameongezeka hadi kufikia zaidi ya wateja 200,000. Sambamba na ongezeko hilo la wateja, imani ya wateja na benki yetu imeendelea kukua na kupelekea amana nazo kukua. Katika kipindi cha miaka hiyo benki yetu imefanikiwa kukuza amana za wateja mwaka hadi mwaka na kufikia bilioni 125 Desemba mwaka jana, huku tukijiwekea malengo ya kufika bilioni 162 mwisho wa mwaka huu.



Zaidi ya mafanikio katika namba, benki yetu imeendelea kuwa kinara katika maswala ya utawala bora. Benki imekuwa ikishinda tuzo mbalimbali ikiwemo tuzo zitolewazo na Bodi ya taifa ya wahasibu na wakaguzi (NBAA) kama mtoa taarifa bora za kifedha katika kipengele cha benki ndogo na za kati miaka 8 mfululizo.

Mwaka 2018 benki yetu ilipokea tuzo kutoka soko la hisa la Dar-es-Salaam (DSE) katika sekta ya benki na uwekezaji chini ya kipengele cha utawala bora ulinzi sahihi wa wawekezaji, utekelezaji bora wa sera za mazingira. Mwaka 2021 benki yetu ilipata tuzo ya *Consumer Choice Awards*, ikiwa ni tuzo ya kwanza kushinda ambapo wateja wetu walitupigia kura kuonesha kufurahishwa kwao na huduma zetu.

### Mwenendo wa Benki

Katika safari hii ya mafanikio, Bodi ya wakurugenzi wa DCB imekua imara na makini kusimamia maslahi ya wanahisa na katika kila hatua kutoa muongozo wenye kuhakikisha malengo ya benki yetu yanafikiwa. Mwaka 2017 Bodi ya wakurugenzi ilipitisha mpango mkakati wa miaka mitano 2017-2022 ambao ulilenga kurudisha benki kwenye faida, kuimarisha mtaji, ukwasi na ubora wa mikopo na hatimaye kuirudisha benki katika ukuaji. Mpango mkakati huu unatekelezwa na matunda yameonekana. Baada ya kupata hasara kubwa kwa miaka miwili mfululizo mwaka 2018 benki ilirudi kwenye faida na hadi leo bado inajiendesha kwa faida.

Benki yetu ipo imara kimtaji,Ukwasi Afya ya kitabu chetu cha mikopo imeimarika ambapo asilimia ya mikopo chechefu imeshuka kutoka asilimia 19 mwaka 2017 hadi kufikia asilimia 7 mwaka 2021 ikiwa ni asilimia 2 tu kufikia kiwango elekezi cha Benki kuu cha asilimia 5.




Mwezi desemba 2020, Bodi ya wakurugenzi ili huisha mpango mkakati mpya wa miaka mitano 2021 – 2025. Mpango huu ulianisha taswira ya mafanikio na jinsi ya kuyafikia mafanikio hayo. Taswira hiyo ya mafanikio inalenga kuongeza faida na hatimaye thamani ya hisa pamoja na ongezeko la gawio kwa wanahisa.

Mpango ambao utekelezaji wake ulianza rasmi mwaka 2021 na mafanikio yake yameanza kuonekana mwaka 2021 faida kabla ya tengo la mikopo na kodi ya mapato shilingi bilioni 4.9 kutoka shilingi milioni 751 mwaka 2020. Faida hii imechagizwa zaidi na kuongezeka kwa mapato kutoka shilingi bilioni 17.5 mwaka 2020 hadi shilingi bilioni 23.3 mwaka 2021.

Hata hivyo mwaka 2021 faida baada ya kodi ni shilingi milioni 798 ikilinganishwa na shilingi milioni 453 mwaka 2020. Faida hii ni ndogo ukilinganisha na ukuaji halisi wa mapato, hii ni kutokana na tengo la mikopo chechefu la kiasi cha shilingi bilioni 3.8.

Ndugu wanahisa mikopo hii chechefu imekua moja ya changamoto yetu ya muda mrefu, ninayo furaha kuwajulisha kwamba mikopo chechefu imepungua kwa kiasi kikubwa kama ilivyotajwa hapo awali. Nimatumaini yangu kuwa tutaanza kuona faida na kutoa gawio kubwa hapo mbeleni.

Vipaumbele vingine vinalenga kukidhi matakwa ya Benki Kuu ikiwa ni uwiano wa mapato na matumizi ya benki (*cost to income ratio*) kufikia aslimia 55 kutoka asilimia 79 pamoja na kiwango cha mikopo chechefu (*non-performing loans)* kufikia asilimia 5 kutoka asilimia 7 mwaka 2021.

Ndugu wanahisa wenzangu, ikumbukwe kuwa ndani ya miaka 20 benki yetu ilifanikiwa kulipa gawio kwa wanahisa mara 15. Haya ni mafanikio makubwa kwa benki na wawekezaji kwani inaonyesha uimara, ufanisi na uthabiti katika uendeshaji wa benki yetu. Kama nilivyoelezea hapo awali, benki yetu sasa imerudi katika kupata faida kila mwaka huku ikiendelea kuimarika zaidi, hivyo ni matumaini yangu kwamba benki itaanza kulipa gawio kila mwaka kama ilivyokuwa desturi yake.

## Shukrani

Baada ya kusema hayo, ningependa kutoka shukurani zangu kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi na wanahisa wetu ambao wameendelea kuwa na sisi na kutushika mkono pale tunapohitaji, iwe ni kuhusu uongezaji mtaji au uhusiano wa kibiashara.

Vilevile tunapenda kuwashukuru wateja wetu wapendwa ambao wanaendelea kuwa nasi katika safari hii, asante kwa kutuamini.

Shukrani za dhati vilevile zinaenda kwa vyombo vyote vya udhibiti, kutokana na usimamizi wao mzuri na mwongozo thabiti pamoja na wadau wengine, ambao kwa njia moja au nyingine wamechangia uwepo wa benki yetu katika miaka yetu hii 20 na tunaamini tutaendelea kuwa pamoja katika miaka mingine ijayo.





**Bw. Godfrey Ndalahwa**
*Mkurugenzi Mtendaji - DCB*

# BARUA YA MKURUGENZI MTENDAJI

Ndugu wanahisa, Mwaka 2020 Bodi ya Wakurugenzi na Uongozi wa benki uliweza kuainisha taswira mpya ya mafanikio ya benki kama ifuatavyo:-

**Wapendwa Wanahisa,**

Kwa niaba ya menejimenti, ninayo furaha kuwaletea taarifa kuhusiana na safari yetu ya benki. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa uhai na afya na kutuwezesha kukutana nanyi tena leo hii.

Tunajivunia mafanikio ambayo benki imeyafikia katika kipindi cha miaka 20 iliyopita toka kuanzishwa kwake, na mimi nichukue fursa hii kupongeza benki yetu kufikisha miaka 20 ikiwa hai, imara na tayari kuendelea kuhudumia watanzania sio tu wa mkoa wa Dar es Salaam, bali nchi nzima.

Ndugu wanahisa, wakati benki inatimiza miaka 20 kwa mafanikio makubwa, ni vyema kuwakumbusha kwamba tumetimiza miaka minne toka tuanze safari yetu ya mabadiliko.

Safari yetu ya mabadiliko iliambatana na changamoto nyingi ikiwemo mtaji wa benki kuwa chini ya kiwango kinachotakiwa, mikopo chechefu kuwa katika kiwango cha juu sana, ukwasiusio ridhisha kwa maendeleo ya benki pamoja na benki kujiendesha kwa hasara. Kwa ushirikiano wenu wanahisa na maelekezo thabiti ya Bodi ya wakurugenzi na juhudi za wafanyakazi wenzangu pamoja na imani ya wateja wetu, tumeweza kukabiliana na changamoto hizi na kwa sasa benki yetu imeweza kujiendesha ikiwa imekidhi kiwango cha mtaji kinachotakiwa kisheria, benki ina ukwasi unaoridhisha,kiwango kidogo cha mikopo chechefu na benki imeendelea kupata faida kwa miaka yote minne mfululizo.



Mimi pamoja na wafanyakazi wenzangu bado tunashauku kubwa ya kuona benki inaendelea kupata mafanikio makubwa zaidi.
Kwa hayo machache sasa naomba kurejea kwenye malengo matatu makubwa ambayo Bodi ya wakurugenzi na wanahisa kwa ujumla walinikabidhi miaka minne iliyopita.

## Kurudisha benki kwenye faida

Lengo la kwanza lilikuwa ni kurejesha benki katika hali yake ya kupata faida mwaka hadi mwaka, lengo ambalo ndani ya miaka minne tuliweza kulifanikisha kwa kiwango kikubwa. Aidha ikumbukwe kuwa mwaka 2016/2017 benki ilitengeneza hasara ya jumla ya shilingi bilioni 10.7 iliyotokana na changamoto mbalimbali. Benki imetimiza lengo hilo la kuzalisha faida miaka minne mfululizo, pamoja na changamoto mbalimbali ambazo tulikuwa tunapitia ikiwemo ugonjwa wa UVIKO-19.

Katika kipindi hicho benki ilijikita katika kupunguza gharama za uendeshaji, ukusanyaji wa madeni kutoka kwenye mikopo chechefu, kuwekeza katika mifumo ya Tehama, kuboresha bidhaa na huduma kwa wateja pamoja na kufunga matawi yasio na tija. Hii iliwezesha benki kuanza kupata faida.

## Benki imara na yenye ushindani

Lengo la pili, lilikuwa ni kuhakikisha benki inakuwa imara na kuendelea kushindana. Ndugu wanahisa, katika eneo hili benki ilijikita katika kukuza mtaji, kuongeza ukwasi na kupunguza mikopo chechefu.

Ndugu wanahisa, kiasi cha mtaji kilitetereka kiasi cha kutokidhi matakwa ya sheria ya Benki Kuu. Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati kabisa wanahisa wote, pale tuliporudi kuwaomba mtaji mlituamini na kutupatia. Napenda kuwahakikishia, mtaji wenu upo salama na unaendelea kukua kupitia faida ambayo tumekuwa tukipata kila mwaka kwa miaka minne mfululizo. Pamoja na kutoa gawio mara moja tu ndani ya miaka hiyo minne faida ambayo imekuwa ikipatikana imekuwa ikitumika kuongeza mtaji na kuimarisha benki zaidi. Kutokana na mafikio haya benki imekuza fedha za wanahisa kutoka shilingi bilioni 20.2 mwaka 2018 hadi shilingi bilioni 30.2 mwaka 2021.




Ndugu wanahisa, naomba kuchukua nafasi hii kukiri kwamba tatizo la mikopo chechefu limekuwa changamoto katika sekta ya fedha kutokana na mabadiliko ya kiuchumi na hasa janga la UVIKO-19. Kama benki kwa miaka minne mfululizo tumeweza kupambana na hii changamoto na kwa kiasi kikubwa tumeweza kulimaliza. Nina furaha kuwaeleza kuwa benki yetu ilifanikiwa kupunguza mikopo chechefu kutoka asilimia 19 mwaka 2017 hadi kufikia asilimia 7 mwaka 2021. Na ni matarajio yetu kwamba mwisho wa mwaka huu 2022 benki itafikia kiwango cha asilimia 5 kinachoelekezwa na Benki kuu na hivyo kuruhusiwa kutoa gawio kwa wanahisa pindi faida inapopatikana.

Ndugu wanahisa, pamoja na kupunguza changamoto hii ya mikopo chechefu kwa kiasi kikubwa, hii ndio imekuwa chanzo kikubwa cha faida yetu ya kila mwaka kwa miaka minne mfululizo kuwa chini ya matarajio yenu.

Katika kipindi cha miaka minne tumeweza kutoa mikopo yenye jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 200 na urejeshaji wake mpaka sasa ni asilimia 99. Vilevile katika kipindi hicho tumeweza kukusanya kiasi cha shilingi bilioni 8 katika mikopo chechefu.
Ni imani yetu kuanzia mwaka huu tutarajie kuona faida inayokidhi matarajio yenu wanahisa na hivyo kuendeleza desturi yetu tulio kuwa nayo hapo awali ya kutoa gawio zuri mwaka hadi mwaka.

Kadhalika, suala la ukwasi kwenye benki ni jambo muhimu sana ni sawa na damu kwenye mwili wa binadamu. Mwaka 2018 amana zilishuka hadi kufikia shilingi bilioni 75 kutoka shilingi bilioni 90 mwaka 2017. Hii ilitokana na baadhi ya wateja kupunguza imani kufatia benki kupata hasara kwa miaka miwili mfululizo. Kutokana na mpango mkakati tuliojiwekea tumeweza kurudisha tena imani kwa wateja wetu na hivyo tumefanikiwa kuongeza amana kutoka shilingi bilioni 75 mwaka 2018 hadi kufika shilingi bilioni 125 mwaka 2021. Ndugu wanahisa, ieleweke kwamba bila kuwa na ukwasi wa kutosha, benki haiwezi kutoa mikopo, kulipa amana za wateja pindi zinapohitajika, pamoja na kutoa gawio.

## Ukuaji na upanuzi wa benki

Lengo la tatu, lilikuwa ni ukuaji na upanuzi wa benki, hata hivyo kwasababu ya kujikita zaidi na lengo la kwanza na la pili, lengo la tatu halikuwa limefafanuliwa vizuri. Hivyo basi, Bodi ya wakurugenzi pamoja na uongozi wa benki ulilazimika kukaa na kujadili upya lengo la mkakati huo. Majadiliano hayo yalikuja kuzaa 'taswira mpya ya mafanikio' na vipaumbele vitakavyo fanikisha kutimiza taswira hiyo.

## Taswira mpya ya Mafanikio

Ndugu wanahisa, Mwaka 2020 Bodi ya Wakurugenzi na Uongozi wa benki uliweza kuainisha taswira mpya ya mafanikio ya benki kama ifuatavyo:

1. Kuongeza kiwango cha faida kinachopatikana kila mwaka hadi kufikia kiasi cha shilingi bilioni 11 mwaka 2025.

2. Kutoa huduma bora zaidi kwa wateja na hivyo kuongeza idadi ya wateja hadi kufikia wateja 400,000 ifikapo mwaka 2025.

3. Kuongeza ufanisi na udhibiti wa mali za benki

4. Kuhakikisha benki yetu inakua mwajiri bora mwenye kuvutia wafanyakazi wenye uwezo na ari kubwa ya kufanya kazi.

## Vipaumbele vitano vitakavyofanikisha taswira mpya ya mafanikio:

1. Kukuza kiwango cha mikopo kwa wateja kutoka kiasi cha shilingi bilioni 104 mwaka 2020 hadi kufikia shilingi bilioni 290 mwaka 2025. Sambamba na hiyo kupunguza mikopo chechefu hadi kufikia chini ya asilimia 5. Mwaka 2021 benki imefanikiwa kukuza mikopo yake hadi kufikia shilingi bilioni 121 ambayo ni sawa sawa na ongezeko la asilimia 16 kwa mwaka. Na pia benki imeweza kupunguza mikopo chechefu kutoka asilimia 11.6 mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 7.3 mwaka 2021.

2. Kuongeza mapato yasiyotokana na riba (non funded income) katika mchango mzima wa mapato ya benki kutoka kiwango cha asilimia 26.4 mwaka 2020 hadi kufikia kiwango cha asilimia 35 mwaka 2025. Lengo hili linalenga kupunguza utegemezi mkubwa wa mapato yanayotokana na mikopo ili kuiwezesha benki kuwa imara zaidi na kuhimili changamoto zinazotokana na mabadiliko ya kiuchumi. Ili kufanikisha lengo hili benki imejikita zaidi kuboresha biashara za bima (bancassurance), huduma za malipo ya kidijitali (GePG, Internet Banking, Mobile Banking, International Money Transfer etc). Benki imefanikiwa kuongeza mapato yasiyotokana na riba kutoka asilimia 26.4 mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 30.8 mwaka 2021.

3. Benki inalenga kuongeza mchango wa amana za gharama nafuu katika amana zote za benki kutoka asilimia 34 mwaka 2020 hadi kufikia asilimia 60 ifikapo mwaka 2025. Nia ya lengo hili ni kupunguza gharama zitokanazo na amana za muda maalumu (Fixed Deposits), ambapo kupungua kwa gharama hizi kutachangia kuongezeka kwa faida na kuleta ongezeko la thamani kwa wanahisa. Benki imeweka mikakati mbalimbali ya kuongeza amana zake ikiwemo kujikita zaidi katika kuboresha na kuleta bidhaa na huduma zenye tija na ubunifu,tutaendelea kuongeza wateja mbalimbali ikiwemo VICOBA, SACCOS, wajasiriamali, wafanyakazi na makundi mbalimbali, kufanya kazi na Mashirika ya simu pamoja na taasisi za serikali.

Benki imeunganishwa na mfumo wa malipo ya serikali (GePG) na imeanza mahusiano na taasisi mbalimbali za serikali zikiwemo manispaa za mkoa wa Dar Es Salaam, Mamlaka ya bandari Tanzania (TPA) na taasisi nyingine za serikali. Mahusiano haya yanatarajia kukuza amana za benki zitokanazo na makusanyo ya mapato ya serikali.

4. Kukuza mtandao wa benki kwa ufanisi – Benki ya DCB imeshaweka lengo lenye shauku la kutoa huduma nchi nzima ifikapo mwaka 2025. Hii itawezekana kupitia muundo wetu wa kibiashara wa kufungua matawi na kusambaza huduma katika maeneo ya karibu kupitia vituo vidogo vidogo na tekinolojia ya kimtandao (*hub and spoke*). Benki inatarajia kufungua matawi mapya 5 na vituo vidogo (DCB Jirani) vipatavyo 28. Kwa sasa benki ina matawi 9 likiwemo tawi letu la Dodoma na tawi jipya la Victoria, vituo vidogo 5 vinavyotumika kutoa huduma mbalimbali za kibenki. Vituo hivyo vipo Dar Es Salaam, Mbeya, Mwanza, Morogoro, na Singida.

5. Benki ya DCB inalenga kuongeza wigo wa mikopo itolewayo kidijitali hadi kufikia asilimia 50 ya mikopo yote ifikapo mwaka 2025. Mikopo hii ni salama zaidi na yenye mapato makubwa na uendeshaji wake ni wa gharama nafuu zaidi ikilinganishwa na mikopo iliyopo kwa sasa. Hata hivyo benki ipo kwenye hatua za mwisho za makubaliano na taasisi mbalimbali zenye mifumo ya teknolojia na makampuni ya simu yenye idadi kubwa ya wateja waliohakikiwa.

Ndugu wanahisa, natambua kwamba kufanikisha kwa taswira hii mpya kutaleta furaha kubwa sana sio tu kwenu wanahisa bali pia kwa Bodi ya wakurugenzi na wafanyakazi wenzangu kwa ujumla. Kwa kuzingatia maelekezo ya Bodi ya wakurugenzi sisi wafanyakazi tuna ahidi kufanya kazi kwa bidii, ueledi na ufanisi mkubwa ili kuhakikisha kuwa taswira hii mpya inatekelezwa kwa wakati.



# WASIFU WA WAKURUGENZI



## Bw. Maharage Ally Chande

Ana shahada ya uzamili katika Uongozi wa Biashara kutoka Chuo Kikuu cha Afrika Kusini na ana shahada ya kwanza ya Electroniki na Mawasiliano kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Bw. Chande ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, alichaguliwa kushika nyadhifa hiyo Disemba 2020. Awali ya hapo alikuwa Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi. Bw. Maharage ni mkurugenzi anayewakilisha kundi la wanahisa binafsi. Hivi sasa Bw. Maharage Chande ni Mkurugenzi Mtendaji wa shirika la umeme Tanzania (TANESCO).

## Bi. Zawadia J. Nanyaro



Ana Shahada ya Uzamili ya Utawala wa Biashara katika Fedha na Shahada ya kwanza ya Biashara katika Uhasibu, Shahada zote mbili alizipata Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Bi. Zawadia J. Nanyaro ni mhasibu (CPA (T)) na mkaguzi (CPA-PP) aliyethibitishwa na chama cha wahesabu na wakaguzi Tanzania (NBAA). Mhakiki wa Mifumo ya kitehama (CISA) na Mkurugenzi aliyeidhinishwa kutoka Taasisi ya Wakurugenzi Tanzania. Bi. Nanyaro alijiunga na Bodi ya Wakurugenzi ya DCB mnamo Mei, 2017 kama mkurugenzi anayewakilisha kundi la wanahisa binafsi. Bi. Nanyaro ni makamu mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya DCB. Hivi sasa ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Lilac Lines Tanzania Limited.



## Bi. Sipora Jonathan Liana

Ana Shahada ya Uzamili katika Maendeleo ya Kiuchumi ya Jamii kutoka Chuo Kikuu Huria na Shahada ya kwanza ya Kilimo kutoka Chuo Kikuu cha Sokoine. Bi. Liana alijiunga na Bodi ya wakurugenzi ya DCB mwezi Mei, 2016. Bi. Liana ni Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam na anawakilisha maslahi ya Baraza la Bodi. Amekuwa Mkurugenzi wa Mikoa ya Arusha na Tabora. Kabla ya kuwa Mkurugenzi katika Halmashauri ya Jiji alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa Wilaya za Mkuranga, Monduli na Moshi. Pia alifanya kazi kama Afisa wa Mifugo na Kilimo huko Njombe kati ya 1988 na 2004. Bi. Liana amehudhuria kozi tofauti na warsha fupi katika maeneo mbalimbali. Bi. Liana alikuwa anawakilisha Halmashauri ya Jiji la Dar Es Salaam, baadae Manispaa ya Kinondoni kabla ya kuhaminishwa kwenda Jiji la Tanga.



## Bw. Aron Titus Kagurumjuli

Ana Shahada ya Uzamili katika Utawala wa Elimu, upangaji na sera za elimu kutoka Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Pia ana Shahada ya Sayansi ya Siasa na Utawala wa Umma kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, pia ana Stashahada katika Elimu ya Watu wazima kutoka Taasisi ya Elimu ya Watu wazima na Astashahada ya Ufundishaji ya Daraja A ya Chuo cha Walimu wa Bunda. Kagurumjuli alijiunga na Bodi ya DCB mwezi Mei, 2016. Alikuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni ambaye alikuwa anawakilisha maslahi ya Halmashauri katika Bodi.

## Bi. Pamela F. Nchimbi



Ana Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara, Shahada ya Biashara katika Masuala ya Fedha (*Corporate Finance*) na cheti cha Uzaji wa Dhamana cha Asasi za masoko ya Kifedha (*ACI Finacial Marketing Association*). Pia ana Cheti cha uuzaji wa dhamana kinachotolewa na Mamlaka ya Masoko na Mitaji Tanzania (CMSA). Bi. Pamela ana cheti cha Usimamizi wa Dhamana na Uwekezaji na Mwakilishi wa wauzaji wa Dhamana aliyeidhinishwa na CMSA. Bi. Nchimbi yupo katika daraja la juu katika kuthibitishwa kama Mchambuzi wa Masuala ya kifedha (Chartered Financial Analyst(CFA)). Bi. Nchimbi ni Mjumbe wa Bodi kutoka Julai 2017 akiwakilisha maslahi ya Taasisi ya UTT-AMIS. Yeye ndiye Mkurugenzi wa sasa wa Idara ya Uwekezaji ya UTT katika Usimamizi wa Mali na Huduma za Wawekezaji tangu 2013.



## Bw. Alexander Sanga

Ana shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara, Shahada ya Sayansi katika Sayansi ya Kompyuta, Cheti cha Ukaguzi wa Mfumo wa Taarifa – ISACA, Meneja wa Taarifa Aliyethibitishwa (CISM) – ISACA, Agile Expert Certified Credential (AEC), Scrum Master Certified Credential (SMC), Balance Score Card Professional (BSP), Cheti cha Ithibati cha Udhibiti wa Mifumo ya Taarifa (CRISC) – ISACA na Cheti cha Ithibati cha Uongozi wa Tehama katika Kampuni (CGEIT) – ISACA. Bw. Sanga aliteuliwa kuwa mjumbe wa Bodi mnamo Aprili 2020 akiwakilisha wanahisa taasisi(Mfuko wa Bima wa Taifa - NHIF). Kwasasa ni Mkurugenzi wa Tehama Mfuko wa Bima wa Taifa.

## Dr. Amina Baamary



Ana Shahada ya Uzamivu katika Usimamizi wa Biashara Mahsusi katika Usimamizi wa Mikopo midogo ya vikundi na Kuendeleza wafanyabishara wadogo na wa kati Chuo Kikuu cha Dar es Salaam/Shule ya Biashara Copenhagen. Ana Shahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Biashara Mahsusi katika Fedha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pia ana Shahada ya Kwanza ya Biashara Mahsusi katitka Ushirika na Fedha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Stashahada ya Uhasibu Chuo Cha Biashara. Dr. Baamary alijiunga na Bodi ya Wakurugenzi ya DCB mnamo Agosti 2021 kama mkurugenzi anayewakilisha kundi la wanahisa binafsi. Kwasasa ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam.



### Bw. Cliff Maregeli

Shahada ya Uzamili ya Sayansi katika Uhandisi wa Kompyuta Chuo Kikuu cha Tu Delt, Uholanzi. Shahada ya Kwanza Sayansi katika Uhandisi wa Kompyuta na Teknolojia ya Habari Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Ni mshirika aliyethibitishwa na Oracle (OCA), na Cisco (CCNA,CCNP) na pia ni Mhakiki wa Mifumo ya kitehama (CISA) katika maswala ya kanzidata na mawasaliano kwa ujumla. Bw. Maregeli alijiunga na Bodi ya Wakurugenzi ya DCB mnamo Agosti 2021 kama mkurugenzi anayewakilisha kundi la wanahisa binafsi. Hivi

### Bw. David Shambwe



Ana Shahada ya Kwanza ya Biashara na Usimamizi Mahsusi katika Masoko. Pia ana cheti cha uuzaji wa Dhamana cha Asasi za Masoko ya Kifedha (ACI Financial Marketing Association). Bw. Shambwe alijiunga na Bodi mnamo November 2021 kama Mkurugenzi huru. Kwasasa ni Mkurugenzi Mdhamini Maendeleo ya Misitu katika kampuni ya Gatsby Africa.



### Bw. Francis Kafuku

Bw. Kafuku ni Mhasibu wa Umma (CPA) mwenye cheti cha Ithibati kutoka Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Ndani (NBAA). Ana Stashahada ya Uhasibu kutoka Chuo Cha Uhasibu Arusha (IAA), Diploma ya Juu ya Uhasibu na Cheti cha Uhasibu zote kutoka Chuo Cha Uhasibu Tanzania (Tanzania Institute of Accountancy). Ana elimu ya Juu ya Hesabu za Jumla (Advanced Tally Accounting) na ni Mtaalamu wa Mambo ya Uhasibu (Accountant Technician). Alifanya kazi kama Afisa Malipo Coca Cola Kwanza Limited (2006 – 2007), NMB Bank kama Afisa Mikopo (2007- 2010), Mhasibu wa Mapato na Matumizi Halmashauri ya Bunda (2010 – 2016), Halmashauri ya Kilwa kama Mhasibu wa Wilaya 2017-2018. Mwaka 2017 -2018, Mhasibu wa Manispaa ya Ubungo, na 2018 - 2021 alikuwa Mhasibu wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke. Bw. Kafuku alikuwa Mjumbe mbadala aliewakilisha Manispaa ya Temeke.

### Bw. Godfrey Ndalahwa



Ana astashahada ya Uongozi kutoka GIBS University of Pretoria, ana Shahada ya Uhasibu na biashara kutoka Chuo kikuu cha Dar es Salaam.

Na pia ni mhasibu aliyethibitishwa na Bodi ya wakaguzi wa mahesabu (NBAA CPA – (T)). Bw. Godfrey Ndalahwa alijiunga na DCB mwezi Octoba 2017 kama Mkurugenzi mtendaji, aliteuliwa rasmi katika nafasi hiyo Januari 2018. Ana miaka 20 ya uzoefu wa kazi za kibenki na uhasibu. Kabla ya hapo alifanya kazi KCB Bank (T) kama Kaimu Mkurugenzi Mkuu na Mjumbe wa Bodi wa benki ya KCB Burundi. Bw. Godfrey aliongoza idara ya fedha ya KCB Bank kuanzia 2013 hadi 2017. Akiwa katika nafasi hiyo alihusika katika kubadilisha benki kutoka kwenye nafasi ya hasara hadi kufikia kupata faida.



# SAFU YA UONGOZI





## Bw. Constatine Mtumbuka

*Mkurugenzi Idara ya fedha*

Mhitimu wa Shahada ya kwanza katika uhasibu wa biashara na fedha kutoka chuo kikuu cha UDSM. Mhasibu wa Umma (CPA) mwenye cheti cha ithibati kutoka Bodi ya Taifa ya wahasibu na wakaguzi Tanzania (NBAA)

Constantine Mtumbuka ni Afisa Mkuu wa Fedha katika benki ya Biashara ya DCB, ambapo anasimamia fedha na utekelezaji wa mipango mikakati ya benki. Pia ana uzoefu wa miaka 14 katika Upangaji wa Kifedha, Ufafanuzi, Utendaji, Uendeshaji na Usimamizi wa Mkakati.

Kabla ya kuajiriwa Benki ya Biashara ya DCB, alishafanya kazi katika Benki ya Exim kama Meneja Mwandamizi wa Fedha anayehusika na kukuza na kuendeleza mikakati ya kampuni, upangaji na utendaji wa benki. Kabla ya kujiunga na Benki ya Exim, pia alifanya kazi benki ya KCB kama Meneja wa Fedha - (Mikakati na utendaji wa benki).

Constantine ni kiongozi mwenye uzoefu alioupata ndani ya sekta ya benki. Pia ana ujuzi thabiti wa huduma nyingi za kifedha na rekodi iliyothibitishwa ya kuongoza timu zinazofanya vizuri kibiashara. Mbali na uzoefu wake mkubwa katika sekta ya benki, hapo awali alifanya kazi katika sekta ya utengenezaji vinywaji, Mawasiliano ya simu na Ushauri.

## Miaka 20 ya Idara ya Fedha

Kwa takribani miaka 20, idara ya fedha ya DCB benki imejizatiti kutoa taarifa za mahesabu yalio sahihi kwa viwango vya kimataifa ambayo yanakidhi vigezo na matakwa ya Bodi ya Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu. Ni kutokana na umakini na utendaji bora wa kazi ndani ya Idara ya Fedha ambayo imepelekea kwa namna moja au nyingine kwenye mafanikio ya benki ya DCB.
Kutokana na juhudi za maandalizi ya mesabu kulingana na ubora na viwango vya kimataifa, DCB benki tumeweza kuteuliwa na Bodi ya Wahasibu na Wakaguzi kuwa kati ya washindi watatu wa kwanza kwa mfululizo ndani ya kipindi cha zaidi ya miaka mitano kati ya taasisi za kibenki zenye kutoa taarifa zenye viwango.
Kwa miaka ishirini mali za benki zimekuwa kutoka shilingi 3.05 bilioni mwaka 2002 hadi kufikia shilingi 194.62 bilioni hii ikiwa ni ukuaji wa wastani wa asilimia 26 kwa mwaka.

Ukuaji wa mapato ya benki ni mkubwa kuliko ukuaji wa gharama hivyo kufanya benki kupata faida kwa miaka yote isipokuwa miaka miwili 2016 na 2017 tu. Tumeweza kutimiza mikakati yetu na ukuwaji wa benki kwenye soko la Tanzania lenye benki zaidi ya 40 kwa kutekeleza bajeti ya mapato na matumizi inayofuata mipango ya benki.
Pia idara ya fedha imeazisha kitengo cha kuchambua na kutafiti utendaji wa benki kwa ajili ya kutoa repoti za mwenendo wa benki kwa idara mbalimbali kwenye benki. Nia ya kuwa na kitengo hiki ni kuhakikisha usimamizi wa utendaji na kuboresha utendaji wa benki siku kwa siku.





## Bw. Nelson Swai

*Mkurugenzi wa Idara - Uendeshaji*

Bw. Nelson Swai ni mhitimu wa Shahada ya Uzamili katika sheria za maswala ya habari na mawasiliano(TEHAMA) iliyotolewa na Muungano wa Mawasiliano ya Kimataifa (ITU) & Chuo cha Mawasiliano cha Uingereza (UKTA), amehitimu Shahada ya kwanza katika Sayansi ya Kompyuta na Hisabati iliyotolewa na Chuo Kikuu cha Bangalore, India.

Ni kiongozi aliyethibitishwa na ISO katika usimamizi wa Usalama wa Habari (ISO 27001 Certified) pamoja na kuwa kiongozi aliyethibitishwa na ISO katika usimamizi wa mwendelezo wa biashara(ISO 22301 Certified). Ni mshirika aliyethibitishwa na Oracle (OCA) na (Cisco) katika maswala ya kanzidata na mawasaliano kwa ujumla. Ni mhitimu wa mafunzo ya uongozi wa kiubunifu kutoka CCL(Center for Creative Leadership), vilevile ni mhitimu wa mafunzo ya uongozi na utawala bora kutoka taasisi ya wakurugenzi Tanzania (IoDT).

Bw. Nelson Swai alijiunga na Benki ya DCB mnamo Julai, 2019 kama Mkurugenzi wa Idara ya Uendeshaji na TEHAMA, awali ya hapo, alikuwa mkuu wa idara ya TEHAMA Ecobank Tanzania kati ya mwaka 2015-2019.

Kabla ya hapo alifanya kazi katika kampuni ya simu ya Vodacom kuanzia mwaka 2010 hadi 2015. Nelson anauzoefu wa miaka kumi na mbili katika masuala ya TEHAMA na uendeshaji wa makampuni katika sekta za mawasiliano na benki.

## MIAKA 20 YA IDARA YA UENDESHAJI

Katika kipindi cha miaka 20 iliyopita, benki imefanya mabadiliko makubwa katika teknolojia na huduma zake. Licha ya kuanza kama taasisi ndogo ya kifedha, benki imekuwa ikitafuta njia bora na rahisi zaidi za kutoa huduma za kifedha zinazolenga mahitaji ya moja kwa moja ya wateja wake, kwa unafuu na ubunifu, huku ikichangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi na kuongeza thamani kwa wanahisa.

Katika kutekeleza lengo hili, benki iliwekeza katika mbinu mpya ambazo zililenga ujumuishaji mkubwa wa teknolojia za kisasa zilizoleta ufanisi katika uendeshaji wa kila siku wa benki na ubunifu wa huduma.

Kwa kutumia teknolojia ya kisasa (API-led Banking approach), benki ina mifumo ya kisasa inayochochea ubunifu na uvumbuzi wa ndani (Creativity & Innovation) na kutoa fursa kwa benki kushirikiana na washirika wa kimkakati (Strategic Partners) katika kuunda mifumo inayorahisisha namna wateja wetu wanavyopokea mapato na kufanya malipo, washirika hawa ni kama : Mitandao ya Simu, njia za malipo za kimataifa (VISA, Mastercard), mtandao wa kimataifa wa SWIFT.

Kwa kutumia teknolojia hii ya kisasa, benki imefanikiwa kubuni mifumo mbali mbali ya kibenki kama DCB Pesa (inayorahishsa upatikanajaji wa huduma za kibenki za kufanya malipo na kutuma pesa kupitia simu za mkononi, DCB Jirani (Inayowezesha wateja wetu kuweka, kutoa pesa na kulipia bili kupitia mtandao wa mawakala wetu nchini bila kuja benki). Internet Banking (inayowezesha wateja wetu kutuma pesa na kufanya malipo wakiwa popote duniani kutumia mtandao wa intaneti), Masterpass QR (inayorahisisha malipo ya huduma na bidhaa, kwenye maeneo mbali mbali ya kibiashara kama, Hospitali, Migahawa, Vituo vya mafuta na maduka mbali mbali nchini), DCB Malipo – mfumo unaorahisisha upokeaji wa malipo ya taasisi kwa kutumia control namba, taasisi hizi ni kama mashule, viwanda, hoteli, mashirika ya ndege na biashara nyingine nyingi.

Benki ilijiunga na mfumo wa Malipo ya serikali - GePG – ambao umewezesha wateja wetu kufanya malipo ya taasisi tofauti za serikali kama vile TRA,TPA, TCAA,NIC, Manispaa za jiji la Dar es salaam na Dodoma, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na taasisi nyingine kutumia njia mbadala kama: Mawakala, Internet banking na DCB Pesa, sambamba na maboresho haya ya kihuduma benki imefanya maboresho makubwa katika miundombinu, nishati na rasilimali watu na kuongeza udhibiti katika usalama wa kimtandao katika kulinda amana za wateja wake.

Maboresho haya ya kimifumo, hayajarahisihsa tu utoaji na upatikanaji wa huduma zetu kwa wateja, lakini yamekuwa na mchango mkubwa katika kuleta vyanzo vipya vya mapato kwa benki na ukuaji wa mapato kwa ujumla.

Tunaposherehekea kumbukumbu ya miaka 20, tumejitolea kuwasikiliza wateja wetu zaidi ili kuendelea kutatua changamoto zao kibunifu na ndani ya wakati ili kufainya benki yetu DCB kuwa kinara kwenye soko, huku tukiendela kukuza ustawi wa jamii iliyotuzunguka na Uchumi wa nchi kwa ujumla.



## MWENDO WA KIDIGITALI



## Bw. Isidori John Msaki

*Mkurugenzi wa Idara - Mikopo*

Mhitimu wa Shahada ya Uzamili katika Ujasiriamali na Uendelezaji wa Biashara Ndogo Ndogo, kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Shahada ya Kwanza ya Sanaa katika Uchumi kutoka Agra, India. Ndugu Isidori amehudhuria kozi mbalimbali za usimamizi wa usimamizi wa mikopo katika taasisi, utoaji huduma wa mikopo, ukusanyaji, urudishaji madeni na uongozi.

Ana miaka 23 ya uzoefu wa shughuli za kibenki. Akifanikiwa kufanya kazi benki ya Akiba Tanzania kuanzia mwaka 2000 mpaka 2007; Nyadhifa alizoshika; Afisa Mikopo, Meneja wa Tawi, na Meneja wa Huduma za Kifedha na mikopo kwa wajasiriamali. Alifanikiwa kuanzisha huduma bora za utoaji mikopo kwa wateja na kufundisha Maafisa Mikopo kuhusu njia bora za ukopeshaji, tathmini ya mikopo, usimamizi na urejeshaji wa mikopo.

Pia, alihudumu katika benki ya Barclays Tanzania (ABSA Tanzania) kuanzia mwaka 2007 mpaka 2010; Mkuu wa Kitengo cha Utoaji wa Mikopo ya wateja binafsi na SME akiwa Barclays aliweza pia kuanzisha Kituo cha kutoa Mikopo nchini pia aliweza kufanya kazi kwa karibu na Kundi la Makampuni la Barclays na kuanzisha Kadi maalumu kwa ajili ya Mikopo isiyokuwa na dhamana (score card) katika benki hiyo. Alifanya kazi na benki ya NBC kuanzia mwaka 2010 mpaka 2017; akiwa Meneja wa Wajasiriamali wadogo wadogo kwa miaka 2 na baadae kuhudumu miaka 5 akiwa Mkuu wa idara ya utoaji wa mikopo ya wateja binafsi na SME. Aliweza kuunda Idara ya Mikopo na kuajiri watu wenye vipawa stahiki sambamba na kufanikiwa kuweka michakato inayoleta matokeo tarajiwa ya mikopo.

Ndugu Isidori aliweza kuwa mwasisi wa mchakato wa kuanzisha mfumo wa kimataifa wa kuangalia viashiria vya mikopo chechefu chini ya mfumo wa kimataifa wa usimamizi uitwao IAS39 kuanzia mwaka 2011 ambapo kwa sasa unajulikana kama IFRS9.

## MIAKA 20 YA IDARA YA MIKOPO

Lengo la kuanzishwa kwa Benki ya DCB lilikuwa ni kutokana na kilio cha wananchi wa mkoa wa Dar Es Salaam kukosa huduma za fedha hasa mikopo kwa wajasiriamali wadogo wadogo hasa wanawake. Baada ya kilio hicho kupitia kwa mkurugenzi wa Jiji la Dar Es Salaam ndipo kiasi cha shilingi billion 1.10 kilipotengwa kwa ajili ya kuanzisha benki ya wananchi wa mkoa wa Dar Es Salaam.

Mnamo mwaka 2002 benki ya wananchi wa mkoa wa Dar Es Salaam ilianzishwa na lengo kuu lilikuwa ni kuwakopesha wanawake wa mkoa wa Dar Es Salaam mikopo midogo midogo kupitia vikundi maalumu vijulikanavyo kwa kitaalamu kama Solidarity Groups au SGL.

Mpango huu uliendelea na kwa kipindi chote cha miaka 20 benki ya DCB iliweza kuwafikia wajasiriamali 45,000 na kuweza kuwapa mikopo yenye thamani ya shilingi billioni 127.7

Pia Benki ya DCB iliendelea kujipanua kwenye upande wa kutoa mikopo kwa kuweza kutengeneza bidhaa za kukopesha wafanyakazi na hasa kwa mikopo maarufu iliyotolewa kwa wanajeshi, polisi na walimu. Hii ni bidhaa ambayo ilipendwa sana kutokana na uharaka wa kupata hii mikopo kwa kipindi cha massaa 24 na iliwezesha benki kuwafikia wateja wake nchi nzima pamoja na kuwa na matawi Dar Es Salaam tu.



## MIKOPO KWA WATEJA WAKUBWA NA WAKATI

Kwa kipindi chote cha miaka 20 benki iliweza kutoa mikopo kwa wafanyakazi wa serikali (Jeshi, polisi, walimu na taasisi nyingine za kiserikali) kiasi cha shilingi bilioni 355.53 kiliweza kukopeshwa kwa kipindi cha miaka 20 mpaka kufikia sasa.

Vilevile kutokana na urejeshaji mzuri kutoka kwa wateja benki iliendelea kupanua wigo wa kutoa mikopo na kuongeza bidhaa nyingine ili kukuza mizania yake na ndipo ilipoanza kutoa mikopo kwa wateja wakubwa na wa kati yaani SMEs.

Mikopo ya wafanya biashara iliongezeka na Benki ya DCB imeweza kujipatia umaarufu kutokana na namna mikopo hiyo inavyotolewa kwa haraka na elimu inayotolewa kwa wajasiriamali kabla ya kupewa mikopo. Kwa kipindi cha miaka 20 tangu kuanzishwa kwa benki imetolewa mikopo ya kiasi cha shilingi za kitanzania bilioni 326.3 mpaka sasa.

Kwa kipindi cha miaka 20 benki ya DCb imepata mafanikio makubwa kwa kuweza kuongeza bidhaa zake za mikopo kwenye soko la wajasiriamali na kuboresha biashara nyingi ambapo wakopaji wengi wameweza kukuza mitaji yao na kukua kiuchumi, benki pia imeweza kutoa elimu ya ujasiriamali kwa wateja wake hasa wale ambao walikuwa wanakopa mikopo ya vikundi maarufu kama SGL.

Kutokana na elimu ambayo inatolewa kwa wateja na wajasiriamali, mikopo imekuwa ikirejeshwa kwa asilimia zaidi ya 98% kwa kipindi chote cha miaka 20 tangu benki ilipoanzishwa. Tangu kuanzishwa kwake, benki ya DCB imeweza kutoa mikopo kwa wajasiriamali wake kiasi cha shilingi bilioni 805.01 na kuweza kuwafikia wateja 164,5000 ambao wamenufaika kwa kupata mikopo kutoka Benki ya DCB.

Tunatoa shukrani za dhati kwa wateja wetu kutokana na kuichagua DCB kufanya biashara na kuweza kupata huduma nzuri na kuitangaza DCB kama Benki inayo mkomboa mteja.





## Bi. Regina Mduma

*Mkurugenzi wa Idara - Sheria na Katibu wa Kampuni*

Shahada ya Kwanza katika Sheria kutoka katika Chuo Kikuu cha Lesotho, Shahada ya Uzamili katika Sheria za masuala ya uuzaji na ununuaji wa bidhaa nje ya nchi (Sheria ya Biashara za Kimataifa) kutoka Chuo Kikuu cha Northwest, Kampasi ya Potchefstroom iliyopo Afrika Kusini na kwa sasa anaendelea na masomo yake ya Shahada ya Uzamivu katika Ufilisi wa Mabenki katika Ukanda wa SADC. Pia, ana Cheti cha masomo ya bima za muda mfupi na mrefu kutoka katika Chuo cha Bima cha Afrika Kusini.

Bi. Regina aliteuliwa kuwa Meneja Mkuu wa Masuala ya Sheria na Katibu wa Kampuni tangu Januari, mwaka 2018. Ana uzoefu wa kitaalamu wa miaka 18katika masuala ya sheria. Amesajiliwa kama Wakili katika mataifa matatu ambayo ni nchi ya Lesotho mwaka 2004, Jamhuri ya Botswana mwaka 2007 na Tanzania mwaka 2012. Regina pia ana cheti cha Makatibu wa Makampuni kutoka Taasisi ya Wakurugenzi Tanzania (IODT).

Kabla ya kujiunga na DCB, Bi. Regina alikuwa anafanya kazi na Kampuni ya Mawakili wa kujitegemea ya Excellent Attorneys Advocates akiwa kama Afisa Mwandamizi wa makampuni na utawala bora na Mkufunzi wa muda mfupi katika Shule ya Sheria ya Tanzania.

Alikuwa akishughulika na makampuni ya biashara, benki na mashirika binafsi na ya umma.

Kabla ya hapo alifanya kazi katika Jamhuri ya Botswana katika kampuni ya Thari Legal Shield T/U Penrich Insurance Brokers, ikiwa kampuni dada ya Benki ya Gaborone. Alianza kama Mshauri wa Sheria na baadae kupandishwa cheo kuwa Meneja wa Huduma za Sheria.

## Miaka 20 ya Idara ya Sheria

Kitengo cha sheria na katibu wa kampuni kilianza na mfanyakazi mmoja (Katibu wa Kampuni) na wanahisa wanne (Jiji la Dar es Salaam, Manispaa ya Ilala, Manispaa ya Kinondoni na Manispaa ya Temeke). Hivi sasa kitengo kina wafanyakazi 6 na wanahisa zaidi ya 7000. Ili kuwahudumia wanahisa wanahisa wake kwa karibu zaidi, mnamo mwaka 2021 benki ilianzisha kitengo maalumu kinachoshughulikia masuala ya wanahisa. Kupitia kitengo hicho wanahisa wanaweza kuhakiki taarifa zao, kupata magawio yao, na kuunganishwa na mawakala wa Soko la Hisa la Dar Es Salaam katika kuuza na kununua hisa. Kupitia kitengo hiki benki imeshuhudia ongezeko la mauzo ya hisa kwa asilimia 256 ukilinganisha na robo ya nne ya 2021 ambapo mauzo yalikuwa asilimia 180.

Kupitia ofisi ya katibu wa kampuni, benki imeendelea kusimamia utawala bora wa kampuni na sheria katika uendeshaji wake. Hivi sasa benki ina Bodi imara yenye wakurugenzi wenye ueledi na ufanisi mkubwa katika masuala ya biashara, benki, udhibiti na teknolojia. Kwa miaka minne mfululizo benki imekuwa ikishinda tuzo za utawala bora zinazotolewa na soko la hisa la dar es salaam. Hii imeifanya benki kuwa kinara katika tasnia ya benki kwenye masuala ya utawala bora. Zaidi ya ya hayo, Bodi na menejimenti ya DCB ina uwiano wa asilimia hamsini kati ya wanawake na wanaume. Sifa hii inaendelea kuifanya benki kuwa kinara katika utawala bora kwa kuzingatia mchango wa wanawake katika endeshaji wake



Benki imejikita katika kuhakikisha inashinda mashauri yaliyoko mahakamani kwa kutumia wanasheria wa ndani ya benki na pia kwa njia ya kutafuta suluhisho mbadala la utatuzi wa migororo. Kwa kutumia njia hii benki imepunguza gharama za kutumia mawakili wakujitegemea. Asilimia 80 za kesi zinasimamiwa na wanasheria wa ndani wa benki hivyo kupunguza gharama za kutumia mawakili na kuongeza kasi ya kumaliza mashauri yaliyoko mahakamani.



## Bi. Doreen Joseph

*Mkurugenzi wa Idara - Hatari na Ikibalii*

Ana uzoefu usimamizi wa hatari akiwa na Shahada ya Kwanza ya Biashara na Usimamizi aliyohitimu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara (Fedha) aliyohitimu katika Shule ya Biashara ya UDSM.

Bi, Doreen alianza kuitumikia taaluma yake katika kampuni ya Kimataifa ya Deloitte and Touché akiwa Mkaguzi wa Hesabu za Nje, Mkaguzi wa Masuala ya fedha na ushauri katika udhibiti wa ndani akikidhi viwango vya kimataifa vilivyowekwa vya udhibiti na ukaguzi wa ndani.Pia, alipata fursa ya kufanya kazi na Kampuni ya NBC LTD (ABSA) inayohusika na Utekelezaji na Udhibiti wa Majanga yenye mahusiano na ile ABSA Capital ya Afrika Kusini.

Alishawahi kufanya kazi na Benki ya Maendeleo ya TIB katika kitengo cha usimamizi wa hatari na sheria, ikiwa ni sehemu ya kufanya mageuzi ya kwenda katika DFI, alianzisha jitihada za usimamizi wa hatari na utekelezaji wakimuundo. Jambo hili lilimpa fursa ya kufanya kazi na IDC ya Afrika Kusini. Kabla ya kujiunga DCB alifanya kazi na Benki ya Twiga katika mizania sawa ya uongozi.

Ana uzoefu usimamizi wa hatari katika biashara ndogo, hatari za kisheria, hatari za uendeshaji wa kampuni, hatari za mikopo, hatari za masoko na ukwasi, Tathmini ya Mradi na Udhibiti wa hatari, mipango mikakati ya kampuni, usimamizi wa utendaji kazi wa kampuni na uongozi kupitia fursa mbalimbali na mafunzo nje na ndani ya nchi.

## MIAKA 20 YA IDARA YA UDHIBITI MAJANGA NA VIHATARISHI

Benki imefikia utekelezaji wake wa mkakati ambao umeweza kuongeza thamani ya benki inayohitajika kupitia mtazamo sawia juu ya fursa na vihatarishi vya biashara. Hili lilifikiwa kupitia mchakato ulioandaliwa rasmi wa mapitio ya kuangalia fursa na changamoto zilizopo katika kufikia malengo ya mikakati.

Katika mwaka wa 2021 benki ilifanya mabadiliko ya udhibiti ambayo yalithibitishwa kupitia kupungua kwa kiasi kikubwa hasara iliyoripotiwa kupitia wizi/ulaghai (Fraud) uliosababishwa na watu na mfumo katika utendaji kazi. Hili liliwezekana kupitia mapitio ya kina ya sera na miongozo ya uendeshaji ambayo ilichangia ufanisi na uboreshaji wa jumla. Bank iliweza kukuza utamaduni ndani ya utendaji kazi kwa kudhibiti vihatarishi kupitia mipango na programu za uhamasishaji.

Bodi kupitia Menejimenti hutumia usawa katika kubainisha viwango vinavyokubalika vya kujua kiwango hatarishi katika kutekeleza malengo ya biashara.




Uzingatiaji wa sheria na utaratibu bado ni eneo la muhimu, benki inatambua uwajibikaji wake kwa washikadau wake wote chini ya matakwa ya kisheria na udhibiti yanayotumika kwa biashara na imejitolea kwa viwango vya juu vya uadilifu na utendakazi wa haki katika uendeshaji wa biashara.

Uthabiti wa mifumo ya benki ulikuwa muhimu katika kupitia mazingira changamano ya biashara, yaani, kubadilisha matarajio ya wateja, maendeleo ya haraka ya teknolojia, changamoto za teknolojia na vitisho vya mtandao. Haya yalisimamiwa ipasavyo katika mwaka huo ili kuhakikisha kiwango cha chini cha athari kwenye malengo ya kimkakati ya benki.



# Bw. Meshack Kayila

*Kaimu Mkurugenzi wa Idara - Rasilimali Watu*

Meshack ana Shahada ya Jiografia na Mazingira kutoka Chuo Kikuu cha Dar-es Salaam.

Alianza kazi August 2012 kama Meneja wa Maendeleo ya Vipaji katika shirika la AIESEC. Juni 2014 hadi Septemba 2015 alifanya kazi kama Mtaalamu wa Rasilimali Watu kampuni ya Favorite HR Service. Kati ya Septemba 2015 na Septemba 2019 aliajiriwa kama Mtaalamu wa Rasilimali Watu na Mshirika wa Biashara Rasilimali Watu Bank of Africa Tanzania Limited. Meshack alijiunga na DCB Commercial Bank Plc mnamo Oktoba 2019 kama Msimamizi wa Rasilimali Watu.

## MIAKA 20 YA IDARA YA RASILIMALI WATU

Benki ya biashara ya DCB ilisajiliwa kwa msajili wa makampuni (BRELA) mnamo mwaka 2001 na iliajiri wafanyakazi 6. Mnamo mwaka 2002 benki hii ilipata kibali cha uendeshaji wa shughuli za kibenki kutoka Benki Kuu ya Tanzania na iliongeza wafanyakazi wake kufikia 15.

Benki iliendelea kukua mwaka hadi mwaka na hivi sasa benki ina wafanyakazi 232. Wafanyakazi wengi wa benki ni vijana, walio na weledi na ufanisi mkubwa katika sekta ya benki. Ajira hizi zinaendana na sera za kuinua vijana na kuongeza wigo wa ajira nchini. Benki inatambua mchango mkubwa uliofanywa na wafanyakazi waanzilishi na mpaka hivi sasa Benki ina wafanyakazi wanne waliokuwepo tangu kuanzishwa kwa benki.

Katika swala la ajira, ingawa wa ajiriwa wengi wa benki ni vijana, benki imeendelea kubadili uwiano wa kijinsia mwaka hadi mwaka ili kuendana na sera zinazohimiza uongozi bora makazini kulingana na uwiano wa kijinsia. Benki ilianza na wafanyakazi wanawake watatu (3) kati ya kumi na tano (15) na hivi sasa ina wafanyakazi wanawake ni asilimia 54.4% Kati ya wafanyakazi 232 walipo kwa sasa.

Hii imesaidia kuleta mahusiano mazuri kazini na kuongeza uaminifu katika utendaji kazi. Kwa kutambua mchango wa wanawake katika uongozi wa benki kuanzia ngazi ya Bodi na menejimenti, benki imeendelea kusherehekea siku ya wanawake duniani mwaka hadi mwaka na pia imetambulika kama benki yenye utawala bora kupitia uwiano wa kijinsia kazini katika sekta ya benki.

Wakati benki imeanzishwa, idara ya fedha ilikuwa imeunganishwa na idara ya rasilimali watu, lakini baada ya benki kukua mwaka hadi mwaka, Bodi na uongozi wa benki ilifanya maamuzi ya kutenganisha idara hizi ili kuongeza uhuru katika utendaji kazi, usimamizi wa kazi na kuhakikisha kila idara inafanya kazi kwa weledi uliotukuka.

Pia idara ya mikopo na idara ya wajasiriamali na mikopo midogo midogo ilikuwa imeunganishwa. Vilevile jinsi benki ilivyoendelea kukua na kuanza kutoa mikopo kwa wafanya bishara wa kati na wakubwa, wafanyakazi wa makampuni na serikali, Bodi na uongozi wa benki uliamua kutenganisha idara hizo. Hii imesaidia sana katika kuimarisha sababu ya kuanzishwa kwa benki hii – kusaidia wafanya bishara na wajasiriamali wadogo (Microfinance) na pia kutoa huduma kwa wananchi wengine.

Kuanzia mwaka 2018 idara ya rasilimali watu ilifanya juhudi kuhakikisha kwamba wafanyakazi wote wa benki wanatambua utamaduni wa kufanya kazi kupitia malengo ya benki na kufanya kazi kwa maadili tuliyojiwekea. Kupitia zoezi hili wakuu wa idara wote ndani ya benki waliteuliwa kama walezi katika matawi yote. Zoezi hili limesaidia sana umoja wa wafanyakazi wetu na kuongeza ushindani katika kufanya kazi na ubunifu wa hali ya juu kazini.

Kupitia idara ya rasilimali watu, wafanyakazi wa benki wameweza kuhudhuria mafunzo mbalimbali ili kuongeza ufanisi kazini. Mafunzo hayo yamesaidia wafanyakazi wetu kuendelea kuaminika na wateja wetu kwenye masuala ya kutoa huduma bora na zinazokubalika katika sekta ya kibenki.

Mwaka 2020 Bodi na menejimenti iliamua kuanza kutoa huduma mbalimbali kwa njia ya kidijitali kwa mfano, mifumo ya kuomba likizo na pia kupata mchanganuo wa mshahara (salary slip) kila mwezi kwa kila mfanyakazi. Benki imeimarisha mawasiliano ya ndani kwa njia za kijiditali na hivyo kurahisisha mawasiliano ya ndani na nje.





# Bw. Deogratius Thadei

*Mkaguzi Mkuu wa Ndani*

Mhasibu wa Umma (CPA) mwenye cheti cha Ithibati kutoka Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi Tanzania (NBAA) na Mwanachama wa Chama cha Wafanyabiashara cha (ACCA-UK). Ana shahada ya kwanza katika uhasibu wa biashara na Fedha kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe.

Huyu ni Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Benki ya Biashara ya DCB tangu Novemba 20, mwaka 2017. Ana ujuzi wa masuala ya ukaguzi wa hesabu za ndani na nje, masuala ya fedha na usimamizi wa akaunti. Fani yake yenye wigo mpana unaoishi mpaka sasa umehudumu katika nyanga za ukaguzi na ushauri katika benki mbalimbali, kampuni za bima na makampuni ya utengenezaji bidhaa mbalimbali.

Kabla ya kujiunga na Benki ya Biashara ya DCB, Deogratius alikuwa Meneja wa Ukaguzi wa Hesabu za Ndani wa Benki ya kwanza ya Taifa ambapo alikuwa anasimamia Idara ya Ukaguzi wa Hesabu za ndani na pia alikuwa na wajibu wa kusimamia miradi ya ukaguzi wa hesabu za benki.

Kabla ya hapo, Deogratius alifanya kazi na Deloitte and Touché akiwa kama Mkaguzi Mshirika mwaka 2011. Alifanikiwa kupanda wadhifa na kuwa Mkaguzi Mwandamizi wa Hesabu za Kampuni akiwa hapo Deloitte.

## Miaka 20 ya Idara ya Ukaguzi wa Ndani

Katika kipindi cha miaka ishirini iliyopita kazi ya ukaguzi wa ndani imebadilika sana ili kuhakikisha kwamba inatoa ushauri wenye lengo la kuongeza thamani kwa biashara ya Benki. Idara ya ukaguzi wa ndani; kiutendaji inaripoti kwa Bodi ya Wakurugenzi na kiutawala kwa Mkurugenzi Mkuu. Kipengele cha ripoti mbili ni muhimu katika kuhakikisha kuwa shughuli ya ukaguzi wa ndani ni huru na yenye ufanisi katika shughuli zake.

Idara inaongozwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani (CIA) ambaye anasaidiwa na timu yenye uzoefu wa kutosha katika masuala ya taaluma, umri na jinsia. Idara ya Ukaguzi wa Ndani huisaidia benki kutimiza malengo yake kwa kufanya ukaguzi na kutoa ushauri wa mbinu zinazoweza kuleta ufanisi katika usimamizi wa masuala ya fedha, udhibiti wa ndani na michakato ya utawala. Idara hutoa shughuli za uhakikisho na ushauri kwa Bodi na wasimamizi wakuu kulingana na kazi halisi ya ukaguzi inayozingatia kanuni, ufuatiliaji endelevu wa biashara na Uchanganuzi wa taarifa.




Idara ya Ukaguzi wa Ndani inatumia mkakati unaozingatia miongozo ya kimataifa ya ukaguzi wa ndani. Mpango wa ukaguzi wa ndani unaendeshwa na tathmini thabiti yenye kuzingatia viashiria hatarishi kwa biashara. Matumizi ya mpango unaozingatia viashiria hatarishi kwa biashara na miogozo ya kimataifa ya ukaguzi wa ndani yana lenga kuhakikisha kwamba malengo ya muda mrefu ya benki na mikakati ya biashara inafanikiwa kwa ufanisi. Huu ni uboreshaji mkubwa kutoka miaka 20 iliyopita.

Mpango wa mwaka wa ukaguzi unazingatia matokeo ya tathmini ya mienendo ya biashara, matarajio ya wawekezaji, mkakati wa biashara, hatari zinazojitokeza katika biashara, mazingira, matakwa ya kisheria na mahitaji ya udhibiti. Aidha, mpango wa ukaguzi wa ndani unaweza kunyumbulika ili kuhakikisha kwamba hatari zinazojitokeza zinazingatiwa na kuingizwa katika shughuli za ukaguzi. Idara ya ukaguzi wa ndani inafanya ukaguzi wake kwa kuzingatia mpango wa mwaka wa ukaguzi ulioidhinishwa na Bodi ya wakurugenzi na kwa kuzingatia mfumo wa Kimataifa wa Kitaalamu katika ukaguzi wa ndani uliotolewa na Taasisi ya wakaguzi wa ndani.

Kwa miaka mingi, idara ya ukaguzi wa ndani imekuwa nguzo muhimu katika kutoa mapendekezo na ushauri kwa biashara na haya yanadhihirika wazi katika uboreshaji wa mazingira ya udhibiti katika miaka mitano iliyopita. Ulaghai umepungua kwa kiasi kikubwa, na miundo ya utawala imeanzishwa ipasavyo. Idara imejumuisha uchanganuzi wa data katika mchakato wa ukaguzi ili kutoa ufahamu zaidi kwa Bodi na Menejimenti. Maboresho ndani ya idara yanafanywa kila siku, ikiwa ni pamoja na matumizi ya teknolojia mpya katika kutekeleza shughuli za ukaguzi, matumizi ya tehama katika kufatilia utekelezaji wa makibaliano baina ya wakaguzi wa ndani na wasimamizi wa biashara na. Haya yote yanafanyika ili kuhakikisha kuwa idara inabaki kuwa muhimu katika kuongeza thamani ya Benki.



## Bw. Zacharia Kapama

*Mkurugenzi wa Idara - Biashara*

Ana shahada ya kwanza katika uhasibu wa biashara na fedha kutoka chuo kikuu cha UDSM. Mhasibu wa Umma (CPA) mwenye cheti cha ithibati kutoka Bodi ya Taifa ya wahasibu na wakaguzi Tanzania (NBAA), Cheti cha Utendaji wa kimkakati na usimamizi(ESAMI).

Bw Zacharia Kapama kwa sasa anafanya kazi pia kama Meneja Mkuu wa Biashara wa DCB Commercial Bank akiwa na majukumu ya kutoa mwelekeo wa kimkakati kuiwezesha benki kufikia malengo na dhamira zake. Ana uzoefu wa jumla ya miaka 13 katika Udhibiti wa fedha, Ripoti za fedha, Ukaguzi na Mikakati; miaka 11 kati yake akifanya kazi katika nafasi za juu za uongozi.

Kabla ya kujiunga na DCB Commercial Bank, alifanya kazi kama Meneja Biashara na Mikakati katika TIB Corporate Bank Ltd; akiwajibika kuimarisha utendaji wa benki na pia kutoa uongozi katika kufuatilia na kudhibiti utekelezaji wa mikakati, pamoja na majukumu mengine. Kabla ya hapo, alifanya kazi KCB Bank Ltd na Barclays Bank kama Business Performance Manager.

Katika miaka mitano ya kwanza, alifanya kazi Deloitte (assurance) na Coca Cola (Mkaguzi Mkuu wa Ndani). Kapama aliiwezesha kuanzishwa kwa mpango mkakati wa miaka mitano ya TIB Corporate Bank na baadae kusimamia utekelezaji wake kati ya 2015 na 2017.

Kabla ya hapo, aliboresha kwa kiasi kikubwa taarifa za usimamizi na jukumu la utendaji wa biashara katika benki ya KCB kupitia mfumo wa usimamizi wa utendaji binafsi na kuanzishwa kwa jukumu la kushirikiana na biashara. Akiwa Benki ya Barclays, aliweza kuboresha kwa kiasi kikubwa umiliki wa akaunti na mchakato wa kupitia mchakato wa upatanisho, kuwapa watumiaji mafunzo na kuhamasisha mradi huo.

## Miaka 20 ya Kitengo cha huduma kwa wateja wa kibiashara

Azma ya kupanua Benki ya Wananchi ya DSM kuwa Benki ya biashara ilipewa kipaumbele mnamo tarehe 31 March 2012 wakati benki ilipofikia mtaji wa Shilingi 14.7. Benki ya DCB ilifungia rasmi kuwa benki ua kibiashara tarehe 2 April 2021 hili lilifanyika kwa kuzingatia faida mbali mbali ikiwa ni pamoja na kufungua dirisha kwa wateja wakubwa (corporate customers) ili kuboresha ukuaji wa benki kimtaji na kutumia fursa nyingi zaidi ambazo benki hapo awali haikuwa na nafasi kuzitumia, kujitanua kimtandao kwa kufungua matawi mikoani kila inapobidi na hivyo kuongeza mapato kwa benki.

Pamoja na kutoa huduma zaidi za kibenki ambazo hapo awali benki haikuwa na fursa ya hii ililenga katika kuongeza thamani kwa benki na kwa wanahisa.

Kwa kuzingatia faida hizo basi kitengo maalumu cha biashara kilijikita kuhakikisha Benki inatoa huduma zoote za kibiashara pamoja mikopo ya muda mrefu, mikopo ya muda mfupi, biashara ya kubadili fedha za kigeni ila Benki hakubasilisha dira na jukumu lake katika kutoa huduma za kifedha katika miradi midogo midogo nay a kati kwa mfumo wa vikundi wa Microfinance.

## Miaka 20 ya Kitengo cha huduma kwa wateja wa binafsi

Kitengo cha huduma kwa wateja binafsi kimekua na kuendelea kushamiri katika kipindi cha miaka 20 tangu Benki yetu kuanzishwa. Benki ilipoanzishwa, kitengo hichi kilijikita hasa katika utoaji wa mikopo kwa wafanyakazi wa serikali. Mikopo hii imekua ikitolewa kwa ufanisi wa hali ya juu ikiwa ni ndani ya saa 24 tangu kujazwa fomu na kukamilika kwa viambatanishi vyote. Ufanisi ambao umekuza kitabu chetu kufikia TZS bilioni 66 mwaka 2021. Mbali na mikopo iliyotolewa kwa wafanyakazi wa serikali, Benki imekua ikitoa mikopo ya ujenzi wa nyumba kwa watu binafsi na hadi kufikia mwaka 2021 kitabu cha mikopo hiyo kilifika TZS bilioni 65.5 Ikiwa ni mchango wa benki yetu katika kuboresha maisha ya mtanzania.

Benki pia imekua mstari wa mbele katika kubuni bidhaa na huduma mbalimbali ili kuhakikisha inawafikia wateja wake popote walipo, na kurahisisha namna wateja wake wanavyopokea na kufanya Malipo yao. Mwaka 2002 benki ilipoanzishwa njia ya kutoa huduma ilikua kupitia tawi lake moja la Anatoglou na ATM za UMOJA switch zilizopatikana kipindi hicho. Ndani ya miaka 20 benki imefanikiwa kufungua matawi 9 (8 Dar es salaam na 1 Dodoma) Pamoja na kuongeza wigo wa ATM za VISA zinazo patikana ndani na nje ya nchi.

Kutokana na mkakati wa kibiashara wa miaka mitano (2017-2022) na (2021 -2025) Benki ilijidhatiti kufikia viwango vya kimataifa vya kibiashara. Utekelezaji wa mikakati hiyo umepelekea Benki yetu sasa kutoa huduma kama vile Internet banking, VISA, Mobile banking (DCB Pesa) Pamoja na huduma nyingine jumuishi za kidigitali zitolewazo kwa kushirikiana na wadau wengine katika sekta ya fedha na mawasiliano. Huduma hizi ni kama vile:



- MasterPass QR – inayomrahisishia mteja kufanya malipo maeneo mbalimbali kama vile migahawa, vituo vya mafuta, maduka ya jumla na kadhalika.
- DCB Malipo – Mfumo unaorahisisha upokeaji wa Malipo ya taasisi kwa kutumia control namba. Taasisi hizi ni kama mashule, hoteli, mashirika ya ndege na biashara Nyingine nyingi.
- Malipo ya GePG – inawezesha wateja wetu kufanya Malipo kwa taasisi tofauti za serikali kama vile TRA, TPA, NIC, Manispaa za jiji la Dar es salaam, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na taasisi Nyingine.

Bidhaa na huduma hizi zimesaidia kukuza amana za wateja kutoka hadi kufikia bilioni 66 in 2021.Benki yetu imeendelea kujidhatiti kukuza amana hizi kupitia kampeni mbalimbali kunadi bidhaa za amana kama vile bidhaa yetu ya fixed deposit iitwayo "Lamba Kwanza", bidhaa zetu za kuweka akabi kwa malengo zikiwa ni "Weka Akiba kwa Hiari (WAHI)" na "DCB Skonga". Bidhaa Nyingine ni kama Akaunti za wanafunzi, mishahara na akaunti za wastaafu. Hizi ni chache tu katika ya bidhaa lukuki tulizonazo.
Benki yetu inaendelea kuimarisha huduma zitolewazo na mawakala wetu nchi nzima tukiwa na matarajio ya kuwepo mikoa yote ifikapo mwaka 2025.



## Bi. Haika Machaku

*Mkurugenzi wa Mikopo Midogo Midogo*

Ana Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Biashara (MBA) na Astashahada ya Masomo ya Elimu ya Juu ya mikopo midogo midogo (PGDMF) zote akizipata kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM). Ana Stashahada ya masuala ya kibenki kutoka Chuo cha Benki (TIOB).

Haika Machaku- Meneja Mkuu wa Mikopo midogo midogo. Ana uzoefu wa zaidi ya miaka 25 katika sekta ya benki, miaka 10 katika nafasi ya utawala. Ana uzoefu mkubwa katika biashara za taasisi za kifedha na huduma za mikopo midogo midogo.

Alishiriki mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi; ikiwemo Taasisi ya Wakurugenzi Tanzania ((IODT), udhibiti majanga na mitazamo ya kiusimamizi, mafunzo ya kimataifa ya huduma za kibenki za simu za mkononi na mawakala yaliyofanyika katika Shule ya Masomo ya Fedha Kenya, safari za mafunzo ya biashara ndogo na za kati yaliyofanyika India na Bangladesh.

Pia alihudhuria mkutano wa kuangalia mustakabali wa uwezeshaji wa wafanyabiashara wadogo na wa kati wa wakurugenzi wakuu na viongozi waandamizi, ubadilishanaji uzoefu wa biashara ndogo na za kati uliofanyika Instabul, Uturuki, Semina ya mafunzo ya uwezeshaji wa mikopo kwa ajili ya nyumba yaliyofanyika katika Chuo Kikuu cha Pennsylvania kilichopo Philadelphia, Marekani, uwezeshaji wa mikopo kwa ajili ya nyumba kwa kaya maskini iliyofanyika katika Chuo cha Huduma za Mikopo midogo midogo cha Boulder kilichopo Turin, Italia, mengine ni usimamizi wa mikopo, tathmini ya mikopo, mauzo na huduma kwa wateja.

Ni mtaalamu wa huduma za kibenki na alifanya tafiti mbalimbali za huduma ya utoaji wa mikopo midogo midogo, mfumo wa kumbukumbu na taarifa za mikopo pamoja na utatuzi wa changamoto za mikopo.

Utafiti wa kwanza ulikuwa unahusu athari za taasisi za huduma za mikopo midogo midogo katika kupunguza umaskini, sampuli ya Dar es salaam Community bank (DCB), 2007.

Utafiti wa pili ulihusu utendaji kazi wa ofisi ya taarifa za mikopo; sampuli ya Chama cha Mabenki Tanzania (TBA), 2010 na utafiti wa mwisho ulikuwa ni Athari za Usimamizi wa Changamoto za Mikopo katika Utendaji wa benki; sampuli ya Benki za kibiashara Tanzania, 2014.

## Miaka 20 ya Idara ya Mikopo Midogo midogo

Kwa kutambua uwezo wa sekta ndogo ya fedha katika kupunguza umaskini na kukuza uchumi, Serikali ya Tanzania ilitunga na kupitisha Sera ya Taifa ya mikopo midogo midogo mwaka 2000 (STM, 2000).

Sera hiyo ilipitiwa mwaka 2007 kwa kutunga Sera ya Taifa ya mikopo midogo midogo ya Fedha ya 2017 (STM, 2017) na mkakati wa utekelezaji wake kwa kipindi cha miaka kumi. Lengo kuu ni kukuza ushirikishwaji wa kifedha kwa kuweka mazingira wezeshi katika sekta ndogo nchini ambayo inaweza kuhudumia mahitaji ya kaya na kuinua kipato cha wajasiriamali wa chini na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi, uzalishaji wa ajira na kupunguza umaskini. Aidha, Serikali ilipitisha sheria ya huduma za mikopo midogo midogo ya fedha ya mwaka 2018.



Benki ya DCB ilianza kutoa huduma ya mikopo midogo midogo mwaka 2002 katika mfumo wa vikundi, ambapo wateja wanaoaminiana hujiunga na kikundi cha watu watano na kuunda senta yenye vikundi kumi. Wateja hupitia mafunzo ya wiki nne kabla ya kupata mikopo. Dhamana ya kwanza ya mkopo ni umoja wao wa kuhakikisha kila aliyekopa ndani ya kikundi anarejesha kwa wakati, wateja hao hukutana kila wiki ili kurejesha mikopo yao. Mikopo midogo midogo ni moja ya alama za benki na kwa kipindi cha miaka ishirini benki ilitoa zaidi ya TZS. 200.0 bilioni kwa Watanzania 400,000.

hapa Dar es salaam; kwa sasa benki imefungua vituo 6 vya kutoa huduma kwa wajasiriamali wadogo katika mikoa ya Morogoro, Mwanza, Singida, Tegeta, Mbeya na Kondoa. Mikakati ya miaka mitano ni kufikia kanda mpya na kuendelea kutoa huduma kwa kufungua vituo 28 vya huduma nchi nzima, kuongeza ufanisi wa uendeshaji na kutoa huduma za kimkakati Pamoja na kuanzisha bidhaa za kipekee na za kiubunifu na kuwa suluhisho kwa watu wa kipato cha chini.

# TAARIFA YA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHA 2021



**Bw. Constatine Mtumbuka**
*Mkurugenzi Idara ya fedha*

## Taarifa ya Fedha ya Mwaka Ulioisha 2021

**Ndugu Wanahisa,**

Ifuatayo ni taarifa ya fedha iliokaguliwa ya mwaka wa fedha ulioishia 31 Disemba 2021 ambayo imegawanyika katika maeneo makuu manne;

- Taarifa ya mapato na matumizi
- Taarifa ya waraka wa mizania
- Taarifa ya mabadiliko ya mtaji
- Taarifa ya mtiririko wa fedha

### Taarifa ya mapato na matumizi

Ndugu wanahisa, Benki ilitenegeneza faida ghafi ya shilingi 4.89 bilioni kabla ya tengo la mikopo na kodi ya mapato ukilinganisha na shilingi 752 milioni mwaka 2020. Baada ya tengo la mikopo chechefu na kodi benki ilibaki na faida ya shilingi 798 milion ukilinganisha na shilingi 453 milioni mwaka wa 2020.

Faida hii ilitokana na mapato na matumizi yafuatayo:

**Mapato ya Riba** – yaliongezeka kufikia shilingi 27.6 bilioni kutoka shilingi 22.7 bilioni mwaka 2020 (22%). Ongezeko hili limetoka na ongezeko la mikopo ya wateja kutoka shilingi 98.1 bilioni mwaka 2020 na kufikia shilingi 117.4 bilioni mwaka 2021 (20%).

**Gharama za Riba** – ziliongezeka kutoka shilingi 9.6 bilioni mwaka 2020 mpaka kufikia shilingi 11.5 bilioni mwaka 2021 (19%). Ongezeko hili limetokana na kukua kwa amana za wateja kutoka shilingi 99.5 bilioni mwaka 2020 mpaka kufikia shilingi 125.3 bilioni mwaka 2021 ikiwa sawa na ongezeko la asilimia 26.

Benki imeweka mikakati ya kupata amana za riba nafuu ili kuendelea kupunguza gharama za riba na kuongeza mapato yanayotokana na riba.

Jumla ya mapato yasiyo ya riba yaliongezeka kutoka shilingi 4.6 bilioni mwaka 2020 na kufikia shilingi 7.2 bilioni mwaka 2021 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 55%. Ongezeko hili limetokana na ongezeko la makusanyo ya ada kwenye mifumo yetu ya kidijitali, mapato ya uendeshaji wa akaunti, mapato ya fedha za kigeni pamoja na ada za dhamana za kibenki (bank guarantees). Pato hili limeweza kuongezeka baada ya benki kuweza kukidhi viwango vinavyoruhusu kufanya miamala ya fedha nje ya nchi kupitia benki ya nje inayoshirikiana nayo (*correspondent bank*).

| (Tsh. Kwa Milioni) | 2021 | 2020 | Badiliko |
|---|---|---|---|
| Mapato ya Riba | 27,618 | 22,665 | 22% |
| Gharama za Riba | 11,464 | 9,638 | 19% |
| Mapato yasiyo ya riba | 7,181 | 4,636 | 55% |
| Gharama za uendeshaji | 18,450 | 16,810 | 10% |
| Tengo la mikopo | 3,820 | (264) | 1547% |
| Faida baada ya kodi | 798 | 453 | 76% |

Gharama za uendeshaji ziliongezeka kutoka TZS 16.8 bilioni na kufikia TZS 18.4 bilioni. Ongezeko hili lilitokana na kuongeza kwa tawi moja la benki (Tawi la Victoria), senta za kutolea huduma mikoani, uzinduzi wa mtandao wa kidijitali na uzinduzi wa nembo na mwonekano mpya wa benki. Ndugu wanahisa, licha ya ongezeko hili la gharama za uendeshaji, ufanisi uliongezeka, mapato yaliongezeka kwa asilimia 33 na uwiano wa gharama za uendeshaji na mapato ya benki uliendelea kupungua na kuimarika hadi kufikia asilimia 79 mwaka 2021 kutoka asilimia 96 mwaka 2020.

Ndugu wanahisa, miaka ya 2016 na 2017 benki ilipata changamoto kubwa ya mikopo chechefu kutokana na vyeti feki na hivyo kupelekea benki kuweka tengo kubwa sana la hasara ya mikopo kulingana na sheria za Benki Kuu na kanuni na taratibu za kimataifa za uandaaji wa mahesabu. Hii ilipelekea kuongezeka kwa tengo la mikopo chechefu kufikia shilingi 3.8 bilioni mwaka huu na hii ndio sababu kubwa ya faida yetu kutokuongezeka kwa kiwango kikubwa ukilinganisha na ukuaji wa mapato yetu.

### Waraka wa mizania.

Taarifa hii inaelezea mali za benki, amana za benki pamoja na mtaji. Mizania ya benki iliongezeka kutoka shilingi 172.9 bilioni mpaka kufikia shilingi 194.6 bilioni mwaka 2021. Ongezeko hili linaonekana zaidi kwenye ongezeko la mikopo na vianzio kwa wateja ilioongezeka kutoka shilingi 98.1 bilioni na kufikia shilingi 117.4 bilioni mwaka 2021. Ongezeko hili ni baada ya benki kuwa imetoa mikopo ya kiasi cha shilingi 90 bilioni mwaka 2021 ukilinganisha na kiasi cha shilingi 73 bilioni iliotolowe mwaka 2020. Amana kutoka kwa wateja ziliongezeka kutoka shilingi 99.5 bilioni na kufikia shilingi 125.3 bilioni mwaka 2021.

| (Tsh. Kwa Milioni) | 2021 | 2020 | Badiliko |
|---|---|---|---|
| Mali za benki | 194,622 | 172,880 | 13% |
| Mikopo na vianzio kwa wateja | 117,390 | 98,070 | 20% |
| Amana za wateja | 125,290 | 99,500 | 26% |
| Mtaji | 30,250 | 29,610 | 2% |

### Taarifa ya mabadiliko ya mtaji

Kutokana na faida tuliyopata, mtaji wetu umezidi kuimarika na kuongezeka na kufikia shilingi 30.3 bilioni mwaka 2021 kutoka shilingi 29.6 bilioni mwaka 2020.

### Taarifa ya mtiririko wa fedha

Taarifa hii inaelezea jinsi fedha zinavoingia na zinavotoka benki. Fedha zinaingia kutokana na faida tuliotengeneza, amana tulizopata na mapato ya riba. Fedha inatoka kwenye uwekezaji wa mikopo kwa wateja, malipo ya gharama za riba na uwekezaji kwenye mali za kudumu za benki.

Benki ilifunga mwaka 2021 na fedha taslimu kiasi cha Tsh. 13.7 bilioni kutoka TZS 9.5 bilioni mwaka 2020. Fedha hizi zinatumika kwenye uwekezaji wa mikopo mwaka 2022.

*Maelezo zaidi kuhusu taarifa hii ya fedha yanapatikana katika kitabu cha taarifa nzima ya mahesabu yaliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha ulioisha 31 Disemba 2021.*

Asanteni sana ndugu wanahisa.

# TAARIFA YA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHA 2021

## VIASHIRIA MUHIMU VYA UTENDAJI

Viashiria Muhimu vifuatavyo vya Utendaji Kazi (KPIs) vinafaa katika kupima utoaji wa mkakati wa Benki na kusimamia biashara.

| KIASHIRIA CHA UTENDAJI | Ufafanunuzi na njia ya Hesabu | 2021 | 2020 |
|---|---|---|---|
| Faida ya thamani ya hisa | Pato halisi/ Jumla ya thamani ya hisa | 3% | 2% |
